# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

# (CKRC)

## Verbatim Report Of

## DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL,

## MWINGI NORTH CONSTITUENCY,

## AT MWINGI SECONDARY SCHOOL

ON

7TH OCTOBER, 2002

Final copy

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL - MWINGI NORTH CONSTITUENCY. HELD AT MWINGI SECONDARY SCHOOL 0N 07/10/2002.**

**Present:**

1. Com. Dr. A. A. Nunow - Chairman

**Secretarial staff present:**

1. David Abdulrahman - Program Officer
2. Asha Boru - District Coordinator

The meeting started at 10:55 with introduction by District Coordinator and Com. Dr. A. A. Nunow in the Chair.

**Musili Musyoka**: Tutaanza mkutano wetu wa leo na kabla hatujaanza nitauliza mtu mmoja atuombee. Councillor Marete tuombee tafadhali.

**Cllr. Jeniffer Marete – (prayer)**: (inaudible) Baba tunakushukuru kwa sababu umetuongoza (inaudible) na ukatufikisha hapa. Hebu niseme Baba ni asante, mbele yetu tuko na majadiliano, tuko na mkutano ingawaje Baba tutajadiliana saa hii, Baba uwenasi. Baba tunakuomba tufanye haki, Mungu tupatie rehema zako, Umungu wako Baba tuuone tukiwa hapa (inaudible)

Saa hii Baba tunakuomba kwa shangwe na ni kwa jina la Yesu Kristo Baba tumeomba na tume amini.

**Audience**: Amen.

**Musili Musyoka – District Coordinator**: Yangu yatakuwa machache. Kwanza nataka kumjulisha kwenu, Commissioner ambaye ametoka Nairobi kuja kujiunga na sisi siku ya leo. Commissioner Abdulrazik Nunow, ndiye Commissioner amejiunga na sisi kuja kutujulisha mpango ambao tunao kwa siku ya leo, ambao ni mpango wa kupokea report ambayo imetokea ya matokeo ya Katiba pamoja na ile Draft Bill. Report ya Katiba na Draft Bill, ambayo itatupatia nafasi ya sisi wananchi wa Mwingi kuanzisha debate juu ya report hiyo ni Draft Bill, ili tujitayarishe kwa mkutano ule mkubwa ambao utakua huko Nairobi kwa National Constitutional Conference.

Kwa hivyo bila kukawia, Bw. Nunow hawa ndyo wananchi wa Mwingi ambao umewahi fika hapa Mwingi Secondary School. Nafikiri wale wengi wanatoka mbali mbali na wako njiani. Wanajua tuko hapa Mwingi na walijulishwa kwa njia mbali mbali, wajiunge na sisi hapa, wangali wako njiana, lakini kwa sababu saa zimeenda, tutaendelea na hawa wako hapa, tukiwangojea wale wengine.

Naona wametoka mbali, wengine wametoka pande za Nuu, wengine wametoka pande za Tseikuru, wengine wametoka pande za Nguune. Kwa hivyo wale wachache ambao wamefika ndiyo tutaendelea nao. Kwa hivyo ningemuuliza bila kukawia, Commissioner wetu Bw. Nunow aendelee na mpango ambao ulituleta hapa kwa sababu tumechelewa sana.

Yeye mwenyewe alikuwa aanze saa tatu unusu kulingana na saa yake, lakini tukachelewesha tukingojea watu na tukingojea mpango huu. Kwa hivyo nitamuuliza aendeshe kile kipindi kingine cha mpango huu. Kwa hivyo Com. Nunow tafadhali.

**Com. Nunow**: Asante sana Bw. Coordinator kwa hayo. Ningependa kuwashukuru nyinyi kwa kufika, natUmmaini kwamba wengine pia watajiunga nasi tukiendelea, lakini kwa sababu ya mahitaji ya muda, itatubidi tuaanze, tuweze kuelezea kuhusu reporti na kuhusu mswada wa kikatiba pia, tukisubiri wengine. Lakini kabla sijaendelea zaidi, ningependa kuwajulisha wenzangu ambao wametoka katika Tume, wafanyi kazi wa Tume, ambao nimekuja nao na ambao pia wana shughulika na mambo fulani kuhusu kazi hii.

Kwanza kuna Bwana Daudi ambaye ni Program Office kutoka Tume na kuna Bii Asha ambaye pia ananasa sauti ya kila neno ambalo litazungumziwa kwa siku ya leo. Ningependa kusema kwamba madhumuni yangu ni kuwaelezea kwa ufupi tumefanya nini baada ya kuzunguka nchi nzima. Kuna Ma-Commissioner ambao walikuja hapa kuchukua maoni yenu sivyo? Na hivyo ndivyo tulienda katika kila Constituency katika taifa hili na katika vikao visivyo pungua mbili katika kila Constituency, tumeketi tukawasikiza. Na baada ya kuchukua haya maoni, haya maoni yote yale yamezungumziwa kwa mdomo, yale yalikuwa yameandikwa kama orodha, memorandum, na yale yametumwa kwa posta, yote yamekusanywa pamoja, yakawa analyzed,

yakaandikwa, tukatengeneza reports, files nyingi sana tukaenda nazo Mombasa. Tukakaa kule mwezi mmoja, tukiwa tunaandika mswaada na reporti hii. Na tulijaribu ilivyo wezekana kuhakikisha kwamba maoni ya wananchi yote yawe katika reporti and at least kama 40% iwe kwenye mswada.

Hii ni kwa sababu Katiba ni chombo ambacho kinaonyesha njia za kupita na ambayo haisemi maneno mengi zaidi, ile tu yale ambayo yanaitwa general principles. Lakini reporti ndiyo inakuwa na maneno zaidi. Na hii reporti vile mnavyo ona nafikiri kuna copies kwa ofisi ya Tume ya District Coordinator, inaitwa short versiyon. Na kuna ya Kiswahili pia. Hiyo ni reporti ambayo imefupishwa kwa sababu reporti hiyo ingine ni kama page 600, 700. Watu wengi wakiona kwa volume tu, wanaweza kuwa discouraged waachane nayo. Na ni kwa sababu ya hiyo tulifanya hii kwa njia ya haraka. Hiyo ingine bado iko kwa publisher, haikutoka. Na ikitoka pia itakuja kwa District Coordinator's office, lakini summary ya hiyo yote iko hapa hakuna mambo yeyote ambayo yameachwa ni maneno tu yamepunguzwa.

Pia Draft Bill ni kama page 250, hiyo pia ni kubwa sana lakini highlight yake ndiyo tulizichukua. Zile highlights katika hiyo mswada ndiyo tulizichukua ili mweze kuangalia Draft Bill kabisa, na reporti pamoja kusudi muweze kujadiliana. Kusudi shughuli yote ni kuhakikisha kwamba wananchi wanaweza kujadiliana, wanaweza kuulizana hili jambo linasema hivi ni vipi?, linamaanisha nini?, matokeo yake yatakuwa nini? kama tunasema kama mawaziri na manaibu ya mawaziri wachaguliwe kutoka nje ya Bunge, kwa sababu wananchi walituambia mambo mengi sana kuhusu hayo.

Kama tulisema, chaguo la Provincial Administration wawe wanachaguliwa na raia. Itakuwa aje kina maanisha nini? Haya ni maswali ambayo mnahitaji kujiuliza na kujadiliana, ili wale kutoka hapa ambao wamekuja kwa National Conference, mwisho wa mwezi huu, kwa sababu tunatarajia kwanza hiyo mkutano kabla ya tarehe 30, tarehe 28, 29. Ni sawa kama Bunge haitakuwa imevunjwa, kunaweza kuwa Bunge lilivunjwa. Lakini sisi tuendelee na program yetu sawa sawa kila kitu kitakuwa kule. Lakini Bunge ikivunjwa hiyo Conference haitawezekana, itatubidi tungoje mpaka Bunge lingine liundwe kisha tuitishe hiyo Conference. Lakini kwa sasa katika orodha ya Tume, tuna hiyo mpango ya kuweka hiyo kivuli ya Conference kufikia mwisho wa mwaka huu. Sasa mkisha jadiliana mtaweza kupeana hiyo reporti kwa wale ambao wanaenda kwa Conference. Kuna watu watatu katika kila wilaya.

Na nilioneshwa mama ambaye atakuweko kule mmoja ya hawo mmoja wa hao lazima awe wa kike. Mnaweza kutuma hizo recommendation zenu pia kwa Tume, kabla ya tarehe ishirini, ama kwa mwisho isipite tarehe 20 ili tuweze kuangalia hiyo reporti na tuweze ku-revise Draft hii kabla ya Conference. Hiyo ndiyo sababu tunasema, at least week moja kabla ya Conference, comment yeyote ambayo mtu anasikia sana ni lazima apeane, ni muhimu ifanywe hivyo kabla ya wakati huo.

Katika hii report ambayo nimesema ni summarized, hiyo report ingine ni ndefu sana na ina mambo nyingi zaidi. Kwa utaratibu ule nita fuata, nitaeleza highlights ambazo zimo katika reporti, kisha niulize wale ambao wana maswala ambayo wangependa kufafanuliwa kidogo, maswali mawili, matatu, kisha niwape highlight ya msuada, hiyo Draft Bill, hivyo pia nauliza wale ambao

wangependa kuuliza maswali ama suggestions ama reactions, hiyo ndiyo ile utaratibu ambayo tutakaofuata. Kwa sababu shughuli hii tuliipangia ichukue muda usiyozidi masaa matatu. Kwa sababu watu pia wana shughuli zao. Summary ya hii ilikuwa kwa magazeti kwa Kingereza na Kiswahili na zitakuwa kwenye maktaba ya Tume, Documentation Centre ya Tume hapa ambayo mtaweza participate wakati wowote.

Ukisha sikia pointi fulani ambayo ungependa kuiangalia zaidi, mtaweza kuyaangalia. Katika hii reporti tumetaja mambo ambayo yametajwa na wananchi, kisha tunaandika kile wananchi wamesema kuhusu hilo jambo, na tuliambiwa kila mahali Katiba iwe na utangulizi.

Katika Chapter ya kwanza ni general introduction, jinsi hii Tume imeundwa na mambo ambayo hayako very specific. Lakini katika Chapter ya pili, ndiyo tumeanza kuyazungumzia utangulizi, Preamble. Na tulijaribu katika hiyo Preamble kuhakikisha ya kwamba tunajaribu kusema vile watu walisema, wangependa nini kuona katika utangulizi. Na wananchi walituambia katika utangulizi wangependa kuona kwamba watu ambao ni wa kabila tofauti, dini totauti na mila tofauti waweze kujulikana katika nchi na watambuliwe kivyao. Si walazimishwe kujibadilisha au kubadilishwa.
Nguvu ya watu ambayo ni foundation ya Taifa. Msingi wa Taifa ni nguvu ya watu. Kwa hivyo utangulizi na ninazungumzia kuhusu Sovereignty of the people. Kwamba watu ndiyo wenye nguvu zaidi mbali siyo wachaguliwa wala siyo viongozi. Tarehe ya nchi kuhusu jinsi tulivyo pigania Uhuru na mambo ambayo tuliyapitia kama Taifa, jinsi tungeweza kuendelea mbele, kuunda umoja na tuhakikishe ya kwamba democrasia ama muongozo wa Katiba unafuatwa. Bila watu wowote kuwa wanapewa nafasi nyingi ama wanasamehewa wakifanya makosa, lakini wengine wanachukuliwa hatua. Kila mtu awe sawa na hiyo usawa pia tuna uzungumzia katika utangulizi.

Pia tulizungumzia kuhusu Bunge na wana Bunge wakichaguliwa, tuwe na Nyumba moja ya Bunge ama mbili. Wananchi wengi walitwambia tuwe na Nyumba mbili, kwa sababu hili Bunge limedharauliwa sana kwa sababu wanafanya mambo ambayo wananchi wanaona kama wanaangalia tu masilahi yao. Kujiongezea pesa, kujiongezea marupurupu. Hiyo jambo nafikiri ndiyo iliangamiza wananchi sana, na nidyo kusudi walisema tuwe na Nyumba ya pili, ili uamuzi wa Nyumba ya pili iweze kuangalia wana Nyumba lingine pia. Isiwe tu ni final, chochote wasemalo linapita hivyo.

Jinsi ya kuchaguliwa, ya kupiga kura. Vyama vya kisiasa vinatakiwa kuendesha kazi yao kivipi? Wapatiwe conditions za kufuata ama waachwe tu wenyewe? Wengi walituaambia kwamba hizo vyama viwe vya kitaifa. Kusiwe na vyama vya kikabila, hiyo pia tu inaweza kuandikwa katika hiyo section. Tuwe na Rais na Makamu wa Rais ambaye watachaguliwa pamoja. Tuwe na Prime Minister, Waziri Mkuu ambaye atakuwa na manaibu wake wawili, na pia atakuwa na Mawaziri ambao atawachagulia kutoka nje.

Tuliambiwa serikali iende chini kwa watu, na kwa sababu hiyo katika hii report, tumesema kwamba kuwe na serikali mpaka kwenye jiji la mwisho. Kijiji ni ndogo ile, zile Councils, ambao watajichagua ama wajihusishe jinsi wanavyotaka, halafu baada

ya hiyo tuwe na District Councils na Provincial Councils, ili serikali iwe karibu na watu. Na haya yote yawe ni msingi wa kiserikali.

Kuwe mahakama chini zaidi, at least kuwe na High Court katika kila wilaya. Na kuwe na mahakama katika vijiji ili mtu ambaye yuko (ni Divisiyon gani ama Location gani iko mbali zaidi kutoka mwingi? Tseikuru iko upande gani? Ni mbali sana siyo? Ni karibu na Kora.) Mtu ambaye yuko Tseikuru si lazima aje Mwingi, kuja kutafuta Justice. Kuwe na Kortini ambayo kule akiridhika anamaliziwa. Asiporidhika, aje a-apeal hapa, lakini si mahali pa kuanzia kabisa ni kilometer 100 na zaidi. Kwa sababu ni yule tu ana pesa ndiyo anaweza enda. Yule hana pesa anadhulumiwa na atakaa na hiyo dhulUmma. Ndiyo sababu tulisema serikali ipelekwe chini.

Kuhusu wafanyi kazi wa Umma, twasema wafanyi kazi wa Umma wasiwe watu ambao wanapelekwa pale ama wanapewa vyeo kwa sababu ya upendeleo. Wawe wanapewa hiyo cheo kwa sababu ana haki ya kuingia hiyo cheo, na ana kile kinahitajika kufanya hiyo kazi. Kusiwe Rais akiingia ni watu wake anawapeleka kazi, hayo ni maoni ambayo watu wanatwambia. Na tukasema sasa, katika wafanya kazi wa umma wawe wametoka katika kila sehemu ya nchi hii, usawa. Siyo 80% watoka mkoa fulani na mikoa mingine yote wawe wanagawa hivyo 20% inayobaki. Hayo yote yaangaliwe katika orodha ya wafanyi kazi wa Umma. Kule kuheshimu Katiba kulipatiwa nguvu zaidi na uwezo zaidi, kwamba kuwe na Commission ambayo italazimika kupeleka watu wake mpaka kwenye kijiji. Kama Commission ya Human Rights iwe na representation katika kila wilaya na katika kila Division, ili mtu akidhulumiwa pale chini ana mahali pa kwenda. Wale wa Gender Commission hivyo, hivyo. Wale wa Integrity Commission ambayo mtu akichukuwa rushwa anatakiwa astakiwe huko huko pia. Kuwe na nafasi ambayo wananchi wanaweza kushughulika katika uongozi. Siyo wangojee waletewe uongozi. Wenyewe waweze kujiongoza kwa njia fulani na kuhakikisha kwamba dhulUmma ambayo itatokea, wana mahali pa kwenda, siyo kuwaweka na nafasi ndogo zaidi ambayo hawajui la kufanya wala hawajui mahali pa kwenda wakidhulumiwa.

Judiciary: Mahakama ilikuwa na mambo mengi zaidi. Tulipoandika maoni ya wananchi kuhusu mahakama peke yake ilikuwa 1008 pages. Na wananchi mwanzo walikuwa wanasema hao ambao wako sasa, wote waondolewe. Lakini kama Tume tukaona hiyo italeta vita zaidi, tupunguze. Tuweke nidhamu fulani, tuweke secret code of conduct na leadership code of conduct pia. Hiyo leadership code ndiyo itahitaji mambo fulani, na tulisema wale ambao wanakaa kwa mahakama ambao wangependa kuchukua fursa ya ku-retire, watapewa miaka tano zaidi ambayo hawajafanya kazi, pension ya miaka tano ambayo hawajafanyia kazi.

Ya pili, tulipunguza miaka yao kutoka 74 hadi 65 kwa sababu wananchi walituambia mtu wa miaka 70 na zaidi na hata tuliambiwa mtu akifikisha miaka 70 asiwe akigombea kiti cha Rais. Tuliambiwa Mheshimiwa kama hana shahada ya degree, asikubaliwe. Councillor kama hana Certificate ya Form 4 asikubaliwe kugombea. Lakini tulisema hatutaki kuchukua hayo yote kwa sababu inaweza kuleta chuki na mambo mengine. Tulisema wale ambao wako, kama mtu alikuwa Diwani zamani, hiyo ni qualification ambayo inampatia uwezo, hata kama hana primary school education ya kuendelea ama ya kugombea. Lakini ni

mpaka tuwe na muda huu wa miaka tano wa elections kwa sababu ni transition.

Na ukisema jambo fulani utaonekana kwamba unazuia watu fulani kugombea viti. So ku-avoid hiyo ambayo inaonekana kwamba wewe unaangalia watu fulani, na tuliambiwa miaka ya mtu kugombea kiti cha Urais iwe kati ya miaka 45-75. Tukasema miaka ya chini isiwe ni 45. Tungeweka miaka ya chini kuwa ni 45 wengi wenu wanajua ni nini ingetokea. Kwamba tunamnyima Uhuru Kenyatta agombee kiti. Ingeonekana hivyo hivyo, na tukisema miaka 70, hawezi gombea, tungeambiwa tunamnyima Simon Nyachae, tunamnyima Kibaki, na wale ambao wamefikisha 70 kugombea viti. Tukasema, katika elections hii, zile rules ambazo zilikuwepo ziendelee. Lakini katika elections ambazo zitafuata, miaka 35-70 ndiyo awe Rais.

Madiwani wawe na shahada ya form four, Wabunge wawe na shahada ya degree. Pia nilikuwa nikiwazungumzia kuhusu mahakama. Hiyo leadership code tulisema wale ambao wanataka ku-retire waende retire, hata kama hawajafikisha mia 50 ama 60 ama miaka yoyote. Wapewe miaka mitano zaidi ya pension. Wale ambao hawata-retire siku 30 kabla ya hii Katiba kuwa adapted na ambao hawana mastaka yeyote ambayo yameletwa kuhusu wao. Hawana neno waendelee. Lakini wale ambao hawatachukua hiyo nafasi na ambao wana mastakha kwa Attorney General's Chambers, Law Society of Kenya, Disciplinary Committee ya advocates na nini, basi kutaundwa Tribunal ya ku-investigate na kufuata haya mashtakha.

Ikawa sasa mahakama walichochea ma-lawyers, waende mahakamani kuzuia hiyo kazi ambayo tulikuwa tukiandika huko Mombasa. Tukaendelea kwa sababu hayo mashtaka yalikuwa imesema kwamba tunatumia reporti lingine ambalo hatuna sisi. Siyo hiyo tulikuwa tunaandika lakini tuliambiwa tuna tumia reporti fulani. Kwa hivyo hiyo mashtaka ilituzuia kutumia hiyo reporti lingine, ambalo hatukuwa tunalitumia, hatuijui. Wakasema sawa.
Tukaendelea na kazi mpaka High Court na Court of Appeal Judges wenyewe wakaenda Kortini. Ni mtu ambaye anasema kwamba hii mambo kwa sababu hainipendezi na haitii maanani masilahi yangu, mimi nayakataa. Na kama kila mmoja katika jamii ambae ataona hii reporti inamtoa madaraka, aende kortini, nafikiri Kenyans wengi wangekuwa kortini, kwa viongozi haswa, kwa sababu viongozi ndiyo wanapunguzwa na wananchi ndiyo wanapewa nguvu zaidi. Wawe katika mahakama, wawe katika Urais, wawe katika Bunge, wawe katika mawaziri, hayo yote yanahusu kupeana nguvu zaidi kwa wananchi wa kawaida. Ili viongozi wawe wanatoa huo uongozi kutoka kwa watu, siyo kujipatia uongozi, ama kuonekana umetumwa kutoka kwa watu na wewe uwezo wako wako unatokama na wengine wala si watu.

Mambo kuhusu ardhi tumesikia zaidi pia, na mashtaka ya ardhi. Na wananchi wamesema Land Registrars wako mbali sana, wangependa iwe karibu na watu. Land Boards iwe ni wananchi wa pale ambao wanaketi na siyo viongozi wa Land Boards. District Land Board awe D.C. hayo yote tuliambiwa na tukayaandika na tuka- recommend, kwamba wananchi wenyewe wa sehemu fulani wajihusishe na mambo ya ardhi. Na tume-recommend kwamba kuundwe Land Commission. A permanent Commission ya kama watu saba ambayo itaendelea na kuangalia mambo ya land katika taifa hili.

Mambo ya urithi na jinsi watu wangerahihishwa kurithi, ni mtoto gani atarithi, ni nani atakuwa anapewa uwezo zaidi kwa

nyumba na jamii na haki ya wasiyojiweza, haki ya wale wamedhulumiwa, marginalized, haki ya viwete, haki ya wanawake. Na tumesema kwa kila Commission ama nidhamu fulani yeyote ya serikali, 33% wawe wanawake kama general principle. Hii ni kwa sababu katika Bunge hili letu la siku ya leo, tuko na wanawake wanane nafikiri ama tisa, kwa watu 222. Na tukisema wanawake watetee viti, watatetea na hawatapata. Ndiyo tulisema kila chama cha kisiasa ni lazima kiweke 33% wanawake kugombea viti, na viti ambavyo wanajua watapata at least half of those, ili tusiweke mwanamke kwa kiti fulani ambacho unahakika hawezi pata chochote, iwe ni mahali hiyo chama ina nguvu. Kama hiyo chama haina nguvu mahali fulani na unaweka wanawake tu kwa sehemu hiyo, hiyo haitakubaliwa.

Tulisema kuwe na mtu ambae atahudumia watu ambao hawawezi kujilipia kodi ya mahakama; Public protector, public defender ambao hiyo ofisi itatoa mtu. Kama unastakiwa kuua mtu, ukipatikana na hiyo hatia utauwawa. Kwa hivyo criminal charges, mwananchi ambae hana pesa, lazima aweze kutetewa, kupatiwa wakili. Kwa sababu kama unadhulumiwa bado uta uwawa tu ukiwa umedhulumiwa.

Electoral Commission tulisema iwe huru na isiwe inachukua amri kutoka kwa mtu yeyote. Tukasema rais awe ndio mchungaji wa Katiba na awe alama ya kuleta wananchi pamoja na ana uwezo mwingi wa kutaja ma-Ambassadors, kutaja Prime Ministers lakini wote watakuwa vetted by Parliament na approval iwe imepeanwa na Parliament.

Kwa ufupi hayo ndiyo mambo ambayo yamo katika hii reporti na zaidi. Na tunaamini mtaweza kupata hii reporti.

**Interjection**: (inaudible)

**Com. Nunow**: Ningeomba muweze kuangalia kabisa.

Ile reporti kamili ikitokea pia ni ya ukurasa 600 na zaidi, mtaweza kuangalia mambo zaidi kule. Lakini yote ambayo yako hapo pia yako kwa hiyo reporti, ila tu hii imefupishwa. Hiyo ina maneno zaidi, kwa sababu gani tunasema hivi? Ikiwa ifanywe hivyo faida yake ni nini? Hasara yake ni nini? Hayo yote yamo katika hiyo ingine, lakini hii ni fupi na inatupatia system ambayo imekuwa summarized.

Pengine ningesimamisha hapo, niulize kama kuna mtu ambaye angependa ku-react tuweze kujadiliana kidogo kabla ya kuendelea tena.

**Charles Mavulya**: Asante sana Bw. Commissioner, nina mambo mawili matatu.

**Interjection**: **Com. Nunow**: Majina tafadhali.

**Charles Mavulya**: Mimi ni Charles Mavulya ambaye ni Mwenye Kiti wa 3C's katika Mwingi North. Nina mambo matatu ambayo nimeonelea ni ya maana sana. Kwanza ni juu ya retirement age ya Judges and other Judicial staff ya miaka 74. Umesema mtu akifikia miaka 70 anaonekana maybe he is a bit worn out. Sasa inafaa nini Jaji awe miaka 74 ama 65, na hali wakati mimi nili-retire nilikuwa 55? Kwani yeye mwana Judge si ni mtu kama mimi? Tena vijana wamesoma sheria, hawapati kazi kwa sababu hawa watu wazee vigongo wamekaa hapo. They should be droped to 55 not even 65. That is my own submission.

Lile lingine ni level of education ya Councillor. Serikali isipoanzia hapo mashinani, Diwani sasa akiwa hajasoma, na nyumba tunajua ni msingi. Sasa Diwani kama hajasoma vizuri. Sasa unafikiri ni serikali gani hiyo ambayo itakuwa kwa haki, itaanza vizuri. Hakuna mwanzo mzuri. Na kwa hivyo mimi naona madiwani wawe wamesoma sawa sawa, kuitafsiri mipango ya serikali na kuona matakwa ya watu yanatumiwa kwa njia nzuri. Wale ambao hawajaelewa mimi nimefanya kazi ya Council for 28 years na nimeona vile udiwani umekuwa, umelete the Government down. Kwa hivyo kuwe na somo kiasi ambayo mtu huyo ataweza kuelewa ni kitu gani kinaendelea.

Lile lingine ni women's representation, eti wapatiwe viti sijui nini. Kwani mmesahau equality na usawa. Si ajitupe uwanjani amenyane na wanaume. Usawa ni nini, kwanza mkisema equality halafu mwanze kusema hatapata. Hatapata nini? Kwa hivyo mimi naona itakuwa ni mambo ingine kutenga kiti ya mtu. Euality, mwanaume versus mwanamke. Si wanasema hivyo. Kwa hiyo haya ndiyo maoni yangu kwamba kama ni kiti tuuwane. Hata leo si wanawake wanapata viti? Kwa hivyo hayo mambo matatu nafikiri tuangalie vizuri kama equality. Nayo itakuwa sawa sawa.

**Com. Nunow**: Asante sana (inaudible).

**Peter Mulava**: Jina langu ni Peter Mulava na mimi ni mmoja katika walimu. Niko na swali moja ambalo linahusu Tume ya uchaguzi. Kama vile Commissioner wamesema eti wasiwe wanatumainiwa na mtu yeyote. Nilikuwa nadhania kwamba ungekuwa a bit precise useme hiyo isiwo chini ya Raisi. Sijui kama hiyo Draft ama hiyo Draft iko precise kwamba huyo Chairman asiwe aki-appointed na mtu fulani badala ya kusema hapo ningetaka tu mwangaza tu zaidi ili tujue kwa sababu tumeona ya kwamba mambo yamekuwa mabaya kwa sababu hiyo Commission ni Executive ndio ina-appoint na hakuna independence katika ECK.

Kile kingine ambacho huyo mzee alikuwa ameuliza, amenibakishia ni jambo la miaka. Ile miaka ya ku-retire. Nafikiri wamesema kwamba hiyo sheria isifwatwe wakati wa uchaguzi ujao. Ambapo tunajua ya kwamba hizi documents zitaenda Bunge. Now my question is, how is the Parliament going to adopt a document leaving some parts of it?

**Com. Nunow**: Inaudible.

**Peter Mulava**: Nauliza hivi--

**Interjection -Com. Nunow**: Rudia hilo swali la pili.

**Peter Mulava**: Hilo la pili, sasa ikiwa hii Draft itaenda Bunge wakati huu, ndiyo maombi yetu. Itakuwa aje kifungu fulani kiachwe nje, kisiwe na effect wakati huu, kiwe effective wakati ujao wa after elections. Kuuliza kwangu ni ikiwa kuna habari ya elimu, habari ya miaka ya retirement, yote its entirety, ipelekwe Bunge, si ati Katiba kuna sehemu zingine ambazo zitakuwa effected some times later?

**Jacob Kitheka**: Jina langu ni Jacob Kitheka. Mimi ni kiongozi wa mmoja katika CPOs zilikuwa zikifanya mafunzo na mimi ni mmoja katika CEPS. Vile vile ningetaka kuzungumza tu juu ya mambo ambayo wenzangu wamejaribu kuzungumza kama vile msemaji aliyetoka alivyosema. Mimi sioni kwa nini tuendelee na jambo ambalo halifai, tukijua ya kwamba halifai, kama vile tulivyojua katika council zetu, zimejaa watu ambao hawajui kusoma. Hawa watu ambao hawajui kusoma sioni kwa nini tusikubaliane kwamba waendelee tu kwa miaka mingine mitano tukijua kwamba hakuna faida watalete. Kama tunawahurumia na kama Tume inafikiria hivyo, na kama wanakenya wengine wanafikiria hivyo, mimi ningefikiria kwamba vile kwamba wewe ulikuwa Councillor haitoshi kwamba unaweza kufanya vizuri. Ningefikiria kwamba ili kumpa nafasi hiyo tu pengine kutengezwe mtihani kama vile Wabunge katika Katiba tuliyonayo wanafanya mtihani fulani na yule ambaye hataweza kupita mtihani huo hafai kuwa Councillor; hatafaa.

Halafu bila shaka tutapata watu ambao wanaweza kusema kitu wakati huu tukiendelea katika hiyo miaka mitano. Lakini kusema tu tuendelee vile tulivyo sasa, Council ambayo watu wawili wamesoma na thelathini hawakusoma, hiyo ni kama Council imetupwa. Imetupwa hiyo, haitaenda na wenzake. Na kama wangekuwa waking'ang'ania kitu kutoka kwa mfuko mmoja, hiyo sasa haitapata kitu.

Kitu kingine ni juu ya umri. Sijui kwa sababu mimi ni mzee watu wengine watasema mimi natetea wazee. Lakini ninaamini kwamba watu kama Ma-Judge ambao wanakuangalia, wanakusikiza, wanaamua unyongwe, nafikiri sikitu ambacho kinafaa mtu ambaye ni mchanga sana. Tunataka mtu ambaye ana umri mzuri. Kwa hivyo mimi nasema kwamba hata kama haitakuwa miaka 74 ifike miaka sabini kwa sababu kuamua tu, hata leo si watu wengi wa-fit, ambao wanaweza kufanya uamuzi mambo yakiwa mazito. Pengine nitaonekana mzee anatetea wenzake lakini hayo ndiyo maoni yangu. Asante sana.

**Com. Nunow**: Inaudible.

**Jennifer Marete**: Bw. Commissioner na wenzangu, mimi ni Jennifer Marete na ni member wa 3 C's Mwingi North Constituency. Yangu ni kama kuuliza, na ni kama ku-comment kwa sababu sijui hapa tunatengeneza Draft ingine ama tunatoa maoni mengine yaende kule, ama ile tulitoa ndiyo ulikuwa unatusomea tuulize ama iko aje? Kwa sababu ni kama sasa tumeanza

kutoa maoni mengine na tayari ni kama tumeandikisha na ikaenda, kwa sababu leo nilikuwa nimesikia ni launching ya Draft ile tulikuwa tume-draft ndiyo iende kwa National Committee. Kwa hivyo sita-amend yoyote lakini niku-comment.

Nikama nasikia ukitusomea vile ile Katiba ambayo tulikuwa tunatengeneza ama tuna-ammend ambayo ilikuwa imetengenezwa hapo awali na wabeberu na muafrika kwa sababu walikuwa wachache. Ndiyo tulikuwa tuna-ammend ndiyo tuwe ruled na Katiba yetu. Ni kama nasikia ya kwamba haitakuwa implemented na Parliament ile sasa tuko nayo, na kwa maoni yangu naona kama hiyo itagarimu sisi hasara kubwa kwa sababu tumewahi kukutana mara nyingi hapa. Tumewahi kuwa na ma-workshop mengi juu ya hiyo Katiba, na hizo workshops na committee zote zilikuwa zinagarimu pesa. Na kila jambo yeyote ilikuwa inaendelea juu ya Katiba, ilikuwa pesa. Na hata kama vile mmesema, kama by the end of this month kutakuwa ni hiyo meeting ya National Conference ( end of tape)

--- zorotesha uchumi kwa hivyo ilikuwa ni maoni yangu, ikiwezekana kwa sababu hii Katiba imechokesha sisi na nyinyi na kila mtu, iwe implemented. Hata ikiwa hiyo Parliament ita kuwa extended at least a month or two months ndiyo hii Katiba itumike kwa sababu tumechoka sana nayo, asante.

**Com. Nunow**: Asante sana (inaudible). Na kabla haujaanza nafikiri ni muhimu tuelewe haswa hiyo intervention ambayo tunafanya ni ya aina gani. Vile mama alisema, siyo ya maoni ni comments kuhusu kuelewa ama kutoelewa jambo fulani; the clarifications, ufafanuzi, ili niweze kueleza zaidi. Kwa sababu kama kutakuwa na reaction, utaweza tu kufanya kama umesha angalia documents kabisa. Na detail ya hiyo document kwa sababu yangu ilikuwa kugusia tu. Endelea.

**Benedict Mulonzia Mulatya**: Asante sana Bw. Commissioner na wenzangu. Mimi naitwa Benedict Mulonzia Mulatya kutoka tarafa ya Nuu. Ni mwana Catholic Justic and Peace na ni member wa (inaudible). Bw. Commissioner, kwanza nafikiria kutoa shukrani kwa kazi muliyoifanya, pengine wengine walifikiria mtamaliza na mkakimbiza kijiti mkakiweka mwisho mlipofikisha Parliament. Ikawa wengine basi wanabaki kubabaika. Mlijikaza kisabuni.

Bw. Commissioner nafikiria kuwa mengi ambayo mulikuwa mfanye yalikuwa yatoke kwetu, nasisi tuliwapa mambo ambayo tunafikiria kuwa yatatufaa leo na kesho na kesho kutwa. Hatukufikiria sana jana ilikuwa aje, hatukujali umri wa Moi tulijua ana-retire, hatukujali umri wa Kibaki au Nyachae. Hatukufikiria habari ya Uhuru Kenyatta, Wewe umesema hapa kuwa mambo mengine mliachilia yaendelee vile yalivyokuwa, ili usifikirike kuwa pengine mnamyima nafasi Uhuru, mnamzuia Kibaki, na mnamzuia Bw. Nyachae. Bwana Commissioner nafikiri ulisema hayo. Sisi wananchi tulivyo keti wakati wa kupunguza miaka na kuipanga, kama mama Councillor alivyo sema, tulichukuwa wakati mrefu sana na tulifikiria kuwa lenu kama Commissioner nikuweka katika Legal language ama kurekebisha hapa na pale.

Lakini siyo kuacha the whole chapter, tukifikiria katika County Councils zetu kama mwenzetu alivyosema na wengine, zimezoroteka kwa sababu the County Councillors most of them wakiletewa hesabu na karani hakuna cha kuuliza ni kupitisha.

Pengine mwenye kiti hatakuwa na nguvu za kuuliza za kujisomea wenyewe. Sasa kama mmeturudisha tulipokuwa, mmetumia pesa nyingi za Kenya, mmetarajia tupange ama pawe na Commission lingine la kuja kuangalia haya? Sisi hatukufikiria waliyo na hiyo. Tulifikiria kuja kuuliza na ikasemekana vile ilivyo Bw. Commissioner. Hapo nafikiria pengine kabla hamjatoa the final Draft muende mketi tena muangalie je wananchi watafikiriwa ama namna gani? Kwa sababu naona hiyo kazi mliyofanya yote Bw. Commissioner.

Kazi tuliyofanya yote nafikiria kama mmefanya hivyo kwingi ingawa mimi nafurahia kwingi hakukufanyika hivyo, lakini mlipofikia wakati wa elections, basi mkaanza pengine kutetemeka kwa sababu mlisemekana hivi, mmefanya hivi, hapo nafikiri mlitukosea kidogo. Kwa sababu ni kikupa Draft yangu inasema at 65 years Jaji waende nyumbani. Wameongezwa miaka kumi juu ya mwananchi yule mwingine wa kawaida ambaye ana retire at 55 years. Kwa nini at 70 awe mkongwe anakwenda kwa kazi akiwa amejikokota amebeba mkongojo, kwa nini na kuna wengi?

Rais asikae pale kufikia 70 years. Hata 65 years tunasema naye ang'oke aondoke pamoja na Judges. Hiyo nikusema yule ambaye ako within that margin, hatapigania Urais, anakwenda kufanya nini? Basi Bw,. Mwenye kiti hayo ni maoni yangu kuchangia, mimi nilitaka kuchangia. Nilifurahia sana ikitokea kwa magazeti, kutokea tena na tunaona kazi kweli tuliyo ifanya ilifika. Tulikuwa tunaombea kuwa mengine yatarushwa yasifike kule, lakini asante kwa kazi mliyofanya, tafadhali mwende muangalie vilivyo. Jaribu (inaudible) ili the document yenyewe iwe the people's choice. Don't make it Commissioners choice.

**Com. Nunow**: Nitaachukuwa swali moja lingine.

**Hillary Muthui**: Asante. Majina yangu ni Hillary Muthui from KLIT. I am a legal officer with KLIT. Samahani nitaongea kwa Kizungu, Kiswahili changu si kizuri.

I would like to congratulate the Commission for its good work and for presenting a very neat document and for reflecting the people's choice and I would like to emphasize what Mr. Mulatya said about doctoring the people's views by compromising what the people said. The people said it is 65 years, the Commission ought to have said that the people said 65 years. They should not doctor the Draft inorder to please certain people. They should tell us the truth. What did the people say, that is what we appointed you to do.

However I understand the fear of the Commissioners of compromising and such; but it should have come out that, this is what the people said, we feel that it should be this way because of this and that for purposes of transition and stuff like that.

You said that the Commission ensures that people who are appointed by government come from all areas and that there will be equal representation of government appointees. How will this be ensured because I can't see it from the draft constitution?

The other thing is that how will ensure that the government will not say that we don't have resources to implement the

Constitution because you say that every District at least ought to have a High Court? How will you ensure that the government does not say that we don't have resources to set up High Courts in every District or to set up all these offices?

The other one was on women representation. You say that each political party ought to have certain number of women standing for elections. How practicable is it? Well I have to talk from ignorance, I would have wanted to benefit from the reasons why you said this and how they arrived at this maybe from the full report, but I would like to have some clarification on this.

I am happy to see that one of the duties of the citizen is to be acquinted with the Constitution but again here I take issue with this because it is also we have observed that the government has been keeping the people in the dark about their rights, about the Constitution. How will it ensure that the people get copies of the Constitution or people know what the Constitution is? I cannot see it from the Constitution itself.

Then you also said that the political parties also should not be tribal based. Again notice that in the present, I am not sure, but I would like to ask you to point out for me how the Constitution ensures that the political parties will not be tribal based. What Constitutional safe-guards are there in the draft that ensure that the political parties will not be tribal based? Thank you.

**Com. Nunow**: Na ya mwisho?

**Joseph Mutonga**: Thank you very much. My names are Joseph Mutonga, I have got three areas that I would like you to clarify and before you do so much as I should tell you, we are told that some Commissioners were derailing the efforts of the Commission, how do we know that the Commissioner infront of us was not one of those Commissioners, but then, I would like you to clarify to us the issue of appointing Ministers out of government. We know from experience that every time we have a Parliament, we usually have a pool of resources of very qualified people in all fields, sometimes even surgeons. So why should we go out of Parliament, to get Ministers out of Parliament, while we can get all the resources or the best brains in Parliament at any one time? It looks suspect to us and considering what the Kenyans are used to of the politicians being promoted from Honorary MPs to Minister, why should we have a system that does not promote MPs Ministers. It looks suspect to me.

May be you would explain to us the rationale or the principles that you are using here. Then perhaps you would also explain to us on the devolution of powers. The draft is very clear on the devolution of powers, on the Province, the District and the Locational level. But then the people are the village level and the Draft is very silent on two issues, that there are no village administrators and that the villagers are tossed to (inaudible) on the mode of government at the village level which raises a very big problem.

We may have as many systems of administration at the village level as we have villages in this country. How comes that the

Draft is not giving us the system of government at the village level, where we have the people? How come the Draft from the Location to the Province, but then it tells us that the people will decide of the mode of government and at the same time we don't even have an administrator at the village level and this is where we have people.

And then lastly I would like you to explain to us if it is true Kenyans said or is it a creation of this Commission that we are going to have 90 nominated MPs? Were these views given by wananchi of this country? Is it true really that this is what we said? Thank you.

**Com. Nunow**: Inaudible.

**Alex Musili**: Thank you very much Mr. Commissioner. My name is Alex Musili, I have been a Civic Education Provider and I have some concerns on the Draft Constitution. One it has actually been talked about very much by colleagues.

One in this Draft Constitution actually it doesn't state why the qualifications that we are talking about and also it doesn't state and there is no where we can see the issue of the MPs in the Constitution.

Two, I think that I listened to the views which have been presented all over the country and there had been an outcry of creation of an office of an Ombudsman and actually when I looked at the Draft Constitution I did not see it, so I don't know whether it is in a different edition or it has been omitted or probably the views were not enough to have colleted to make that office of the Ombudsman.

**Com. Nunow**: Asanteni sasa, nafikiri hata mimi ningekuwa more comfortable nikizungumza Kingereza lakini nitajilazimisha kuzungumza Kiswahili na pengine ni mix saa zingine kusudi wale hawaelewi waweze kuelewa.

Kuhusu comment ya miaka ya kustaafu ya ma-judges, ilikuwa 74 tukaipunguza kuwa 65 years na tulisikia maoni mengi sana. Haya maoni ambayo tulisema ni maoni ya watu na ni rahisi sana watu kuhakikisha kwamba kama kweli ni maoni ya watu ama ni maoni ya ma-Commissioner. Tumetengeneza Constituency report ambayo hii ni ya Mwingi North Constituency. Na baada ya nafikiri either week hii kama hazijafika tayari, kutakuwa na copy ya kila Constituency, katika kila Documentation Center, 210 na mwananchi anaweza kwenda hapa aziangalie zote, ahakikishe hiyo ambayo imeingia hapa ni maoni ya watu, ama si maoni ya watu. Kwa sababu kila Constituency ni 1 out of 210 na pengine jambo fulani ambalo halikutokea Constituency fulani, limetokea katika Constituecy zingine nyingi. Ndiyo kia Constituency kutakuwa mambo ambayo hawajasema, ambayo yamo hapo. Na jinsi mtakavyo kuhakikisha tu ni kuangalia Constituency report yote.

Ma-Judges wengine walituambia wakae hiyo miaka 74, wengine walisema wapunguzwe kwa miaka 55 wengine miaka 60,

wengine 65, wengine 70. Hizi miaka zote zimetajwa. Na ikawa hiyo 65 years ndiyo compromise ya hayo ambayo inakaribia karibu zote.

Elimu ya Ma-Councillors ambayo inapatikana na zingine nyingi pia. Kuna jambo tunaita transitional provision na hayo katika kila Katiba ambayo itaandikwa dunia nzima. Kwamba hii Katiba ingekuwa imeandikwa 1998, ambayo ingekuwa adopted 1998 or so, ni mapema sana hamuingii katika elections miaka nyingi ijayo. Lakini unaingia uchaguzi baada ya mwaka mmoja wa Katiba kuchukuliwa ama chini wa mwaka mmoja kama wakati huu ambao tunaingia katika elections, watu wengi hawatakuwa wameelewa hiyo Katiba, hiyo ni hakika. Haitapata nafasi ya kufika mashinani, wengi watakuwa wamesikia tu; kuambiwa. Lakini kama una miaka mitatu mine ambayo Katiba imechukuliwa na una mika mitatu mine kabla ya uchaguzi, wengi watakuwa wameijuwa. Na ni kwa sababu hiyo kama wakati wa kwandika Katiba umekaribia, wakati wa uchaguzi ni lazima kuwe na transition provision.

Na kuhusu miaka ya elections ya ofisi ya uchaguzi ambayo inaendelea wakati huu, wa Kidiwani na ya Bunge, tuliyaweka katika Transition Provisions. Na ni kwa sababu hiyo ndiyo tunasema,kwa wakati huu, hiyo Transition Provision applies to ile ambayo ilikuwa inaendelea. Siyo kwamba sehemu hiyo ya Katiba haitachukuliwa. Itachukuliwa, kwamba Rais awe katika katikati ya miaka 35 na 70, lakini Transition Provision ndiyo inaleta qualification ya hiyo clause, ambayo inasema kuwa this Transition kutakuwa na uchaguzi wa Udiwani na Bunge na Rais na itafanywa jinsi ilivyokuwa zamani kuhusu miaka. Ni Transition Provision ambayo ni wakati huu tu itatumika kwa sababu Transition ni kwamba itakuvukisha na baada ya hiyo imetoka. Lakini iko pia katika Katiba, inachukuliwa pamoja kwa hiyo Draft.

Tume haikuogopa mtu yeyote, wala kutishwa na njia yeyote ile, ni ile tu nidhamu ya utaratibu. Watu wengi hawatakuwa na wameelewa kama Katiba itakuwa adopted by December, na elections ziwe January tuseme, just for an example. Wengi hawatajua kwamba haya mahitaji yamebadilishwa. Both wale wanatafuta ofisi na wale wanapiga kura. Ni ajili hiyi Transition Provision ambayo tuliweka kule si Transition Provision ya elections peke yake. Kuna mahali kadha yenye Transition Provision Clause ambayo mkiangalia hiyo Transition Provision Clause mtajuwa inasema nini.
Kuhusu akina mama, imesemekana wameuliza equality kwa hivyo ni lazima wajitetee kivyao. Hiyo imejaribiwa na ikawa haitowi matokeo, kwa sababu akina mama ni msingi wa nyumbani pia, na kwamba wao ndio wanalea watoto. Mzee anaenda na mama anaachwa nyumbani. Mzee na mama wote wakienda ofisini, Wakifika jioni mzee anaketi, mama anaingia jikoni. Hiyo ni reality ya society yetu ya kiafrika na kimila. Na kwa hiyo nafasi yao inapungua ya kwenda kutafuta kura na kukimbia na ku-travel. Mama leo akisema anaeda kutafuta kura tuseme sehemu za Garrisa. Mzee anaweza kumkataza, aambiwe hapana kaa. Na iliangaliwa kila mahali na sauti ya wanaweke ilikuwa moja kwamba wao wamenyimwa haki nyingi, waliwekwa kando, walitengwa, wapatiwe provision kwamba viti fulani viwe ni viao na kwamba at least iwekwe nadhamu fulani ambayo itawawezesha kuhusishwa katika uongozi na serikali. Na ni kwa sababu hiyo hii general principle ya 1/3 iliwekwa. Na pia Kenya kama nchi imesha sign certifications nyingi, conventions nyingi kutoka Beijing, plus five na zingine ambayo zinaweka haki za wanawake kiasi fulani, specific provisions. Na kama taifa tunalazimika kufuata zile conventions ambazo tunapiga sign.

Tusipige sign mwanzo tulazimishwe, lakini tukisha piga sign mpaka tuangalie kiasi ambacho hakitaharibu Katiba yetu.

Kuhusu Electoral Commission. Yale nilikuwa nikiyataja ni kwa ufupi sana. Lakini kuna jinsi Electoral Commission watakuwa appointed, nimesema hawatakuwa chini ya mtu yeyote yule. Lakini watakuwa appointed by the President using certain qualifications and certifications ambazo zimewekwa kwa Katiba na baada ya hiyo itakuwa vetted by Parliament, kuhakikisha kwamba zile details zimewekwa nadhamu imepatwa na President. Kwa hivyo President hatakuwa anafanya hiyo kivyake. Ya kwanza atakuwa anafuata nadhamu na taratibu fulani, na qualifications fulani. Na baada ya hiyo kuhakikisha kwamba amepata haya itaangaliwa na Bunge.

Nafikiri mama alikuwa amesema Katiba iweze kuwa adopted wakati huu. Hivyo pia ndiyo maombi yetu. Ndiyo sababu mnatuona tukikimbia haraka sana, kwa sababu kila tulipoenda tuliambiwa mharakishe Katiba iwe tayari na msiharibu mkiharakisha. Tulisema kutakuwa na National Constitutional Conference mwezi huu tarehe 28. Na jinsi tulivyo panga hiyo Conference ni ya watu 650 na kati ya hao 250 zaidi ya asilimia 33% ni Wabunge, MPs. Ikawa wao wata cooperate tukahesabu tukaona 1/3 ni watu ambao ni homogeneous wametoka mahali pamoja wote na wana interest moja. Nafikiri tulipangia muda wa mwezi moja. Huo mwezi utatosha. Lakini wao wakiamua kuichelewesha, kwa sababu sisi kama Tume tutakuwa ex-officio members. Tutakuwa makarani tu pale. Hatutakuwa na sauti, hatutakuwa na kura, tutakuwa tunasikiza na kuandika na kuweka ile nidhamu ya watu kuendelea; facilitation. Kwa hivyo tukimaliza hiyo Conference kwa mwezi moja, sisi kwa muda usiyo zidi wiki moja tuta-revise hiyo Draft Bill, tukitumia maoni na recommendations ambazo zimetokea kutoka Conference ambayo ina watu kutoka kila wilaya, ina watu kutoka civil society, ina watu kutoka Bunge, ina watu wa dini, ina watu wa Tribunal, ina watu wa Professional associations. Tutaipeleka bunge baada ya wiki moja. Na Bunge italazimika kupitisha hiyo Katiba kwa muda usiyo zidi wiki moja. Hiyo yote ni kuhakikisha kwamba isicheleweshwe na isilalishwe. Baada ya hiyo wiki moja itaenda kwa Rais na Rais analazimika kuweka kidole kwa muda usiyozidi wiki moja pia yaani siku saba. Na kama Bunge itakuweko, tunaweza kuwa na Katiba mpya kufikia December kati kati. Lakini Bunge ikivunjwa ambayo mlisikia Rais akisema tutaenda kwa uchaguzi kupitia Katiba iliyoko sasa. Namaanisha Bunge ikivunjwa, National Constitutial Conference haitakuweko kwa sababu 33% ya members hawatakuweko na MPs.

Hiyo itakuwa ni lazima kuhairisha hiyo Conference hadi Bunge mpya iundwe kisha waje kwa Conference. Hiyo tu ndiyo ile jambo inaweza chelewesha Katiba mpya. Kuhusu uchaguzi, uchaguzi unaweza fanywa hata mwezi wa nne, kufuatia Katiba iliyoko. Maanake Katiba ambayo iliyoko sasa, haikatazi elections zifanywe December. Kile kinatakiwa ni kwamba Bunge lazima liketi siku tisaini, within ninety baada ya kuvunjwa Bunge. Within ninety days. Wanaweza keti within the the first thirty days or within the second thirty days or within the last week of the ninety days or the last day of the ninety days.

Hili Bunge limeketi mwanzo tarehe 3 mwezi wa February 1998. Mwezi wa pili tarehe 3 ndiyo hilo limeketi, litaweza endelea mpaka tarehe mbili mwezi wa pili bila kuongeza muda, ni haki katika Katiba iliyoko sasa. Na Bunge likivunjwa tarehe 2 lazima liketi within ninety days baada ya tarehe 2 mwezi wa pili. Kwa hivyo inaweza keti kufikia tarehe mbili mwezi wa tano sivyo?

Kwa hivyo uchaguzi unaweza fanywa wakati wowote katikati ya tarehe 2 mwezi wa pili hadi tarehe 1 ya mwezi wa tano. Ndiyo sababu tunasema elections zikifanywa mwezi wa nne, Bunge livunjwe mwezi wa pili mwanzo first uwende campaign, mwezi wa tatu ama wa nne elections zifanywe, Bunge liketi mwisho wa mwezi wa nne. Bado haitakuwa imeongeza wakati wake. It does not need Constitutional amendments ambayo iko sasa. Nafikiri tumeelewana.
Kwa hivyo kama kuna niya ya viongozi kuhakikisha kwamba Katiba mpya iwe msingi wa elections inaweza kufanywa bila Bunge kujiongezea muda.

Nilisema kuhusu Transition Provision, hiyo inahusu mambo ya miaka ya watu. Kwa hakika nilisema pia yale yako hapo, kuhakikisha kwamba ni maoni ya watu ni kuangalia Constituency Report. Kwa hivyo haitasaidia sana nikisema ni maoni ya watu ama si maoni ya watu. Kwamba najua ni maoni ya watu, na kama si ya hii Constituency ni ya Constituencies zingine. Kwa hivyo naomba muweze kuangalia hii Report na zingine za Constituency zingine.

Mwingine aliuliza kuhusu equal representation and how that should be ensured. How the government can be taken to the lower level, how people will know the Constitution, how we can avoid tribal political parties. All these are questions that the Constitution cannot provide details on, but the Constitution can provide mandatory requirements that this can be done. Now facilitation of this will be Legislative issues. Jinsi hayo yataweza kutimizwa itakuwa mambo ya Bunge, lakini italazimika kufanywa. Kwa sababu tulisema Katiba ni guideline tu ya general provisions ambazo zinahitajika kufwatwa. Haitaweza kusema hayo kwa details zaidi lakini ikisemakana kwamba tuseme Judge asiwe kwenye ofisi zaidi ya miaka 65, ni wale wanahusika na hiyo nidhamu wakalazimika kwamba wasimtaje mtu kuwa Judge akiwa amepitisha hiyo miaka. Sivyo?

Lakini Katiba haiwezi kusema jinsi ingehakikishwa kufanya hivyo, ila tu inasema kwamba hiyo lazima ifanyike na hayo ni kama kuna jambo katika Katiba kimekuwa cha lazima, na jinsi hiyo ingetimizwa itakuwa ni mambo ya Bunge kwa sababu Acts of Parliament ina-facilitate the Constitution. Tumesema Bunge inatengeneza Katiba. Kutengeneza Katiba inamaanisha kwamba Katiba ambayo ilitengenezwa iwe inapewa meno ya kuUmma, miguu ya kutembea na jinsi itakayo iwezesha kufanya kazi.

Mwenzangu aliuliza kuhusu Makamishna ambao derail process. Siwezi kujitetea lakini nafikiri nawaachia nyinyi kuamua kama ni mmoja wao ama si mmoja wao, lakini kuna wenzetu ambao walikuwa wanatumiwa kisiasa kuharibu mambo hiyo nina hakika.

Kuhusu kutoa mawaziri kutoka nje ya Bunge, tulielezwa kwa sehemu nyingi sana na kwa kinaganaga sana tena. Kwa sababu ilisemekana Minister kama ni mtu muadilifu sana ambaye ni honest, atakuwa appointed na watu wake kabisa.

Hawamuoni wakifika kule kama hapo ofisi mwake ni security kiasi huwezi pitia. Na hapa haji, hapati nafasi kwa sababu anatumikia nchi nzima. Hiyo ilikuwa shida moja.

Ya pili kama Waziri siyo muadilifu, siyo honest ataleta ile mali ambayo ingetumika nchi nzima katika Constituency yake peke

yake ili achaguliwe tena. Njia mbili zote ni mbaya. Ndiyo tuliambiwa wawe ni professionals wako nje pale na wachaguliwe ni Ministers lakini Bunge I-vett, credentials za hawa watu na history yao. So hiyo ndiyo ilikuwa sababu ilitulazimisha tuweke hiyo recommendation. Kwani kama wananchi wamerudia rudia jambo fulani na waikose kwa Report na kwa Bill inakuwa shida. Yale maoni ambayo haikutajwa mara nyingi, yale maoni yametokeya kwa sehemu chache tu, tuliweka tu kwa report, lakini yale yalirudiwa sana, tuliweka kwa Draft Bill. Pia kuhusu hivi viti tisaini ya proportional representation, tuliambiwa mahili kwingi kwamba watu wa sehemu fulani watu wanapenda chama na sehemu nyingi kwingine, watu wanapenda mtu. Mahali fulani ambapo chama linapendwa lakini wale wamechukua ikiti yake hawakuchaguliwa. Hiyo chama haitakuwa na mtu yeyote Bunge. Kwa hivyo kuna chaguo mbili, kuna chaguo la bahati ambalo ni chama iliwekwa kisheria na la mtu ambae pia ni haki yake. Ndiyo kwa sababu tulisema pia Provision for independent candidate.

Kama mtu chama ilimfukuza na wananchi wanampenda, na haya ndiyo tulisikia, itakuwaaje sasa wananchi wanalazimika kumchagua mtu mwengine kwa sababu mtu huyu mwenye kiti wa chama hampendi ama Secretary General hampendi. Tukasema suluhisho ya hiyo ni independent candidate; na tuna propose kwamba, mtu anaweza kugombania kiti kibinafsi, bila kuwa mwanachama yeyote. Na kama vyama vinachaguliwa, na mtu pia anachaguliwa, chama pia iwe na kura, ili ukienda kwa kura, unawekewa kura moja mtu binafsi ama mtu mwenye chama ambacho anakimbilia, anagombea kiti fulani. Lakini hiyo itakuwa tu ni kura ya wakati wa Bunge. Haihusu Udiwani wala haihusu Urais. Kwa sababu hizi viti tisaini ni vya Bunge. Kwa hivyo wakati unapoweka kura ya MP, unaweka kura ya chama pia. Pengine, mtu anakupenda wewe kama mtu, hapendi chama chako. Kwa policies na madhumuni ya party anapanda chama kingine ambacho kina policy nzuri. Anaweza kupatia chama hicho nguvu na pia akuchaguwe wewe kama mtu, ama akuchaguwe wewe na pia achaguwe chama chako.

Hiyo ndiyo sababu ya hii Proportional Representation. Pia katika Proportional Representation, ambayo inaweza hakikishwa wanawake wapewe nafasi kwa sababu hata kama chama kiliweka watu katika sehemu fulani, ya ugombeaji wa kiti wa MP, pengine hawataweza kuchaguliwa lakini kwa kulazimisha parties kuweka alternate members katika orodha yake ya proportional representation. Ya kwanza kama ni mama ya pili ni mwanamme, ya tatu ni mama hivyo hivyo. Ama ya kwanza ni wa kiume hivyo tena, ili kama hiyo chama imepata 10% of 90 seats goes to that party. Miti tisa katika hiyo tisaini itaenda kwa hiyo chama. Hiyo ndiyo ilikuwa madhumuni ya proposal representation.

Katika swali kuhusu Ombudsman, ni kweli watu wengi walisema kuhusu Ombudsman na nafikiri ni jina ndiyo tunaita People's Protector. Iko katika ofisi ya Human Rights and Administrative Justice. Tulisema badala ya kuweka Commissions nyingi tuweke hiyo Human Rights and Administrative Justice na iwe na departments ya People's Protector Ombudsman, department ya Gender Commission, Departments kadha chini ya hiyo, ili mwananchi akienda mahali fulani asiambiwe umekuja ofisi lingine, hiyo ofisi ya hawa ni mahali fulani. If you put it in one centre you get one stop kind of shopping. Unaenda mahali pamoja, kama unadhulumiwa, kama unatakiwa kutetewa, kama kuna violations una-report, yote unaweza ku-report mahali moja ili Ofisi ya Ombudsman inapewa ile inahusika nayo baada ya kupokea reporti. Kwa hivyo Ofisi ya Ombudsman iko katika hii Draft Bill.

Asanteni sana nafikiri mgeniruhusu ningeendelea, ningegusia kidogo kuhusu Draft Bill na still wengi wenu hawakuona Draft Bill kwa sababu tuli-launch kiharaka sana kwa sababu Ma-Judges walikuwa wanataka kuizuia isitoke kabisa.

Nafikiri kama imefika hiyo Draft Bill pengine ingekuwa na copies chache sana kwa Documentation Centre, but at least kuna copy. So mliona kwa magazeti hiyo pia ni same ni hiyo hiyo tu imekuwa serialized. Kwa sababu wananchi wanahamu sana kujua nini kimekuwa recommended. Lakini jinsi ninavyosema, mjue ni Draft. Inaweza kubadilishwa, inaweza ondolewa, inaweza ongezwa na hiyo itakuwa ni jukumu la National Constitutional Conference. Yangu na ya wenzangu leo ambayo pia tumeenda sehemu zote za taifa hili.

Katika hii Constituency hatutaweza kwenda mahali mbili lakini tunaenda mahali moja ili-tu-stimulate, kuanzisha mueze ku-debate na kuangalia vile vitu, na ninatarajia kutaitwa mikutano ya Constitutional Committees or Constituencies, waweze kuleta watu pamoja, waweze kujadiliana hayo na waweze kufanya informed suggestions. Kwa sababu ni ngumu sana kufanya suggestions kama watu hawakuangalia vizuri ama hawakusoma, ama hawakupatiwa fursa ya kujadiliana. Katika hii Draft Bill tuna onelea nchi yetu ya Kenya, kama nchi ambayo wananchi watahusishwa kiserikali na nidhamu ya kiserikali na maisha ya utaratibu wa kiserikali kwa sababu ina affect mwananchi, lazima mwananchi aulizwe na ahusishwe jinsi atakavyo ongozwa kiserikali.

Bunge lazima liwe chaguo la watu. Bunge isiwe ni Bunge ambayo ina chaguliwa na inawasahau watu. Iwe ni Bunge ambayo inachaguliwa na watu na iko accountable kwa watu. Siyo kwa wengi na lazima Bunge liweze kufanya serikali iwe accountable. Bunge lazima ifanywe Executive kiasi ambacho kinaendesha nidhamu ya serikali iwe accountable na isiwe inachukua instructions kutoka serikali, bali iwe uhuru na iwe inaangalia nidhamu ya serikali kama inaleta madhara kwa raia na wananchi, lazima Bunge liingilie ili kuwe na checks and balances ambazo ziko tofauti kabisa.

Pia katika hii Draft Bill, tulionelea nchi ambayo itakuwa na uwezeo ambao umewekwa kwa mikono mingi tofauti. Isiwe uwezo wote uko katika mikono ya watu wachache ama mtu mmoja. Kusiwe na mtu yeyote ambaye kiviake peke yake bila kuuliza mtu anaweza kufanya vituko ambazo zitaumiza wananchi ama watu wa Kenya.

Vyombo vya serikali lazima ziwe accountable kwa watu. Kila chombo cha serikali kiwe KFC kiwe ni Parastatal ya serikali na kiwe ni Executive, kiwe Judiciary, kiwe Legislative; yote wawe accountable kwa watu. Na waweze kufanya vile wananchi wanaamua waendeshe hiyo kazi.

Watu wa Kenya wote, kila kikundi, kila kabila na kila mtu binanafsi lazima aonekane kama anadhaminiwa. Hakuna mtu ambaye amechagua kuwa kabila fulani for instance, hakuna mtu amechagua kuwa katika jiji fulani, ama sehemu fulani ya taifa. Na kusiwe upendeleo ama chuki kwa mtu kwa sababu ya kabila lake, kwa sababu ya asili yake, kwa sababu ya rangi yake, kwa sababu ya kikundi chake ama chama cha kisiasa chake. Maisha ya binadamu lazima iheshimiwe na uwezo wa binadamu

katika hii taifa lazima ipatiwe nafasi ya kutumika. Profession ya watu lazima itumiwe na mtu apatiwe nafasi ya kutumia mafikira yake, aweze kupatiwa nafasi ya kufanya biashara, nafasi ya kutembea katika taifa, nafasi ya kununua chochote mahali yoyote katika taifa. Na maisha ya binadamu lazima ionekana kama vile iko, sacred. Isiwe mtu yeyote anaweza kuiondoa.

Mahitaji ya misingi ya wananchi lazima kupatikana. Vitu nyingi haziwezi kupatikana overnight ama kwa mwaka, ama kwa miaka mitatu, ama miaka mitano, lakini kama ni mambo ya kikatiba; kila kiongozi ambaye anahusika atawajibika, kutimiza jinsi itakavyo wezekana aendelee kwa hiyo direction. Kwamba mahitaji ya kimsingi kama ya afya, ya elimu, ya nyumba, ya sanitation ni ya afya pia, public health na chakula ya kila mwananchi lazima wale wanaongoza taifa wajihusishe nayo. Na wahakikishe kwamba sehemu moja ya nchi ama watu fulani wa nchi, ama kikundi fulani wanataabika na sehemu zingine ama vikundi vingine wanakaa na mambo nyingi sana zaidi ya mahitaji yao. Na hiyo inamaanisha distribution of resources. So that hamna yule anapendelewa wala hamna yule anaachwa nyUmma.

Maisha ya serikali pia lazima ifuate nidhamu ambayo haina rushwa, iwe ni serikali ambayo inasema corruption haitakikani, na isiwe siyo inataja tu lakini iwe inachukuwa hatua ya kuhakikisha kwamba corruption inaangaliwa; na tunaomba kwamba siku moja tutaiona nchi ambayo corruption itakuwa ni jambo la aibu sana. Ya mtu kuambiwa kuwa huyo amefanya hivi, ameiba mahali fulani, ya shirika fulani ya kiserikali. Iwe ni kitu ambacho mtu angependa asitajwe nayo kabisa kuliko vile sasa tuko na watu wengi wanaabudu mali, ikawa kama una mali haidhuru ulipata aje, bali upate tu mali. Kuwa masikini ndiyo dhambi katika taifa letu leo. Na hiyo ni kukosa ile morality ya ethics, ya binadamu kujua nini mbaya nini nzuri.

Kama ulivuja tuseme Kenya Posts and Telecommunications kabisa, umeimeza, na umenunua mali nyingi ambayo ni Mwingi mara kumi, wewe sasa utakuwa unachaguliwa, utakuwa unaenda popote unapotaka na unaweza kuhakikisha yule unataka ndiye atachaguliwa kwa sababu una mali. Lakini tuseme tulikuwa na taifa ambayo inaona corruption ni mbaya na ni mbaya jinsi ilivyo mbaya, mtu ambaye amepata mali kwa njia mbaya angekuwa anatengwa kabisa. Akose mahali pa kulala, alale mahoteli zake tu, akose bibi wa kuoa kama ni mwanaume, ama mme wa kuoa kwa sababu alijulikana kwamba ni mtu ambaye amepata mali vibaya. Na kila mtu binafsi akianzisha maisha yake, aiangalie kwamba maisha ya taifa ni maisha ya watu kuongezwa lingine. Nafikiri baada ya muda fulani tunaweza fikia kiwango fulani ya kupunguza corruption kabisa. Kama si kuiondoa kabisa.

Vyama vya kisiasa si lazima zikubaliane, lakini tunaonelea wakosane na wamalize mambo yao bila vita. Peaceful settlement of disagreements within political parties. Waweze kujadiliana ama kukubali kutokubaliana, lakini siyo wachochee wananchi na watu wapigane kwa sababu ya tofauti ya maoni ya vyama.

Mali ya taifa: Mali yote ya taifa ikiwemo ardhi, na mali ingine yote, maji ardhi, lazima vitumiwe kwa njia inavyofaa na matokeo katika mali ya taifa, mali asili ya taifa yote iwe imegawiwa katika wananchi wa kila sehemu, kwa jinsi ambayo inafaa wote. Siyo kupeleka mali nyingi mahali fulani na kuachia mahali ingine.

Pia tunaonelea serikali ambayo inapatikana pamoja na watu wa serikali, wawe wanashughulika na ujenzi wa taifa. Serikali na raia wote, wajihusishe na wahusishwe na viongozi kwa mambo ya ujenzi wa kitaifa. Haya yote yamo katika hii Draft Bill, na ina mambo mengi zaidi jinsi kila moja hayo ingeweza kutimizwa. Jinsi wananchi na serikali wangeweza kuhusishwa na wenyewe wangejihusisha na ujenzi wa taifa umo katika Draft Bill.

Jinsi ofisi za Kikatiba, Constitutional offices zingeundwa, nyingi zinahitajika kufuatia hizo Constitutional offices, wakiwemo ofisi ya Tume ya kuweka mishahara ya wafanyi kazi wa serikali wote wakiwemo Wabunge. Kusiwe na mtu yeyote yule ambaye anaweza kuamuka asubuhi na kujiongezea mshahara wake ama marupu rupu yake. Tume ime-recommend Tume ambayo inaitwa Salaries and Renumeration Commission ambayo kazi yake ni kuangalia salaries na other benefits ya wafanyi kazi wa Umma wawe wamechaguliwa ama hawakuchaguliwa, waweze kuangaliwa.

Jinsi watu wangeweza husishwa na mashughuli ya kiserikali na maisha ya Umma kwa kila level pia ina ma-article nyingi sana, mpaka article 30 katika hiyo Draft Bill. Wakiwemo mmoja wao ni Rais achaguliwe na 20% ya mikoa mitano lakini pia awe amepata 50% kwa kura yote ya taifa. Kwa sababu kuna weza kuwa mtu apate kura chini ya ¼, 25% na aweze kupata 25% ya mikoa. Na tulisikia wananchi wakisema 25% ya mikoa haifai peke yake. Kuwe na pia idadi fulani ili mtu anajulikana amechaguliwa na watu wengi zaidi.

Mambo ya mahakama na jinsi mahakama inatakiwa kupelekwa mashinani yote inalazimisha watu wahusike kwa shuguli ya uongozi na kiserikali. Jinsi Bunge ingewezeshwa kwamba ni chaguo la watu na iko accountable kwa watu, na jinsi ingeweza kuhakikisha kwamba inaweka serikali iwe accountable, pia ina deal na articles kama 15, nyingi sana.

Pia kuna uwezo wa uongozi uwe kwa mikono tofauti tofauti, tuna katika hiyo bill jinsi hiyo ingehakikishwa ifanyike. Na kuna hata articles 12 na chapter mbili nzima ambayo yanazungumzia hayo.

Tuna pia swali la vyomba vya serikali ambayo wanahitajika kuwa accountable kwa watu, jinsi hiyo ingeweze kufanyika na ni nini tume-recommend katika Katiba katika hii bill kuhakikisha kwamba hiyo inafanyika, ina articles 24.

Pia watu vikundi na hata binafsi na makabila ni lazima wawe wanadhaminiwa usawa, na wanapatiwa haki ya usawa. Hiyo pia kuna ma-articles mpaka 20 yanazungumzia hayo.

Kuhusu maisha ya binadamu na jinsi maisha ya binadamu inatakikana kuheshimiwa na jinsi inatakikana watu wapewe nafasi ya kutumia ile potential yao kwa manufaa ya taifa. Katika hiyo tuna recommend Commission ambayo inaitwa Economic and Social Council. Hiyo ambayo inajihusiha na mambo ya economy na social na ambayo itakuwa na jukumu ya ku-advise Bunge, ku-advise President na kujulisha wananchi ni nini inafanyika, na kuuliza wananchi ni nini wangependa ifanyike kuhusu kufufua

uchumi na kuiendesha vizuri. Pia kuhusu maisha ya kiserikali na jinsi wafanyi kazi wa kiserikali wanatakikana kupigana na rushwa na wananchi pia wanatakikana kuhusishwa na upiganaji wa corruption, pia tumezungumzia mpaka articles 13.

Political disagreements iwe inasuluhiswha kwa njia isiyo ya vita na uadui pia inazungumziwa kwa urefu sana. Na mojawapo ya kufanya hayo ni ile elections procedure ya proportional representation ambapo kila chama kitakuwa kimetafuta kura kivyake kama chama na siyo kupitia watu ambao wamechaguliwa, siyo tu kwa njia empty. Lakini chama iwe imepata nidhamu fulani so that kila sehemu vyama vyote viweze kwenda kuomba kura. Kama chama hakina the field MPs wa sehemu fulani, haina sababu ya kwenda katika wilaya fulani ama sehemu fulani. Lakini kwa sababu inataka kura ya chama itawajibika kutafuta kura kwa kila sehemu.

Mali asili ya kitaifa kama ardhi na maji iwe imegawiwa wananchi wote kwa njia ya usawa. Hiyo pia kuna articles mpaka 8 yanazungumzia. Serikali na watu, wananchi wanatakikana kuhakikisha wamehusishwa kwa ujenzi wa kitaifa ina articles kama 4 kuzungumzia hiyo mambo na uhakikishe ya kwamba, mambo ya ardhi na ile injustices imefanyiwa kuhusu ardhi kwa miaka zilizopita tangu ukoloni na mbele ya ukoloni iangaliwe na watu siyo Lands Commission tutawapatia jukumu ya kuhakikisha ya kwamba imekuja na land framework ambayo itakuwa iko acceptable kwa wananchi wa Kenya.

Kuna ile Commission ambayo inaitwa Njonjo Commission ambayo inaendelea sasa na tulitaka kupata reporti yao ili tuweze ni nini wameambiwa na wananchi, kwa sababu walienda wilaya tu, ama walienda mikoa tu nafikiri. Lakini sisi tulienda mpaka Constituencies, so nafikiri tulipata information zaidi kuliko wao, lakini walitunyima hata hiyo information ile walipata kwa sababu wanasema wamesign ile Secrecy Act na ni mpaka wapeane hiyo information kwa Rais ambaye aliwa-appoint ndiyo itakuwa public. Ni Rais anaweza kuifanya public. Hizo ndizo Commission nyingi ambazo zimetumia mali ya Umma, zinafanya reporti, zinatumia mali ya Umma zinazunguka mwaka mmoja, miaka miwili na hatuoni, imefichwa imewekwa.

Lakini wale stake holders ambao wamejitolea kutengeneza hii Tume, wanaonelea hiyo na wamekataa kabisa, na ndiyo sababu tulikuwa na stalemate tangu 1997. Lakini baadaye ikawa wamekubaliwa na ikawa kwa hiyo Chapter 3A kwamba hii information yetu ni public. Mtu wa kwanza kupokea kabla ya Rais ni mwananchi na baadaye ni Bunge na ni baadaye Rais ataiona. Kwa sababu wale ambao wameulizwa maswali ambayo wameandika hii Katiba kimaoni ni wananchi, na kama kuna mwingine atatoa maoni yake bila wao kuona ni mbaya. Sisi ni kuhakikisha kwamba ile tumeunda tunawapa nyinyi mnaiangalia na nyinyi ndiyo mtaamua kama ni maoni yenu ama si maoni yenu, si mtu mwingine. Wananchi wakisema hii si maoni ya wananchi, basi itakuwa ni shida yetu na ndiyo sababu haitusumbui sana yeyote askisema ambaye yuko nje kule, aseme hii si maoni ya watu. Kwa sababu maoni ya watu itaamuliwa na watu wenyewe na nyinyi ndiyo mtaangalia hizi reports na mtajua na mtasema kama si reporti yenu ama kama at least pale yale yamesemwa katika hii Constituency yamo kwa Constituency Report na yako katika National Report hata kama part of it haikuenda kwa Draft Bill.

Mambo ya uchaguzi: Bunge iwe na Nyumba mbili ya National Council na National Assembly, hiyo pia tuliyazungumzia sana na

jinsi electoral process ingeweza kufanya kazi. Uchaguzi wa Rais ambao nimegusia sasa, election ya Council kutoka mashinani. Pia kutakuwa na uamuzi kuhusu ni nani ataketi katika chamber ya pili ya Bunge na itafanya nini, kazi yake itakuwa nini, hiyo National Council. Hiyo imeguzwa na mpaka articles 5. Kuhusu jinsi hiyo devolved governement ingeweza kufanya kazi. Jinsi ingekuwa implemented na jinsi ingefanya kazi inaangaliwa na mpaka article saba. Itakuwa na uwezo gani wa kutengeneza sheria, uwezo gani wa kuokota kodi na nini itakuwa ni jukumu la Bunge na Central Government. Inafanya hiyo distinction vizuri sana.

Draft jinsi tulivyo propose inaongeza uwezo ya wanawake katika jamii, na hiyo imezungumziwa na ma-aritcles nyingi zaidi ya 13 kuhusu citizenship for instance. Kama mwananchi wa Kenya ameolewa na mtu kutoka ng'ambo baada ya miaka miwili kuishi nchi hii anaweza kuomba citizenship. Yule kuolewa awe mme awe mke. Kwa wakati huu kama ni mme, anapewa, kama ni mke hapewi. Kama mwanamke kutoka Kenya ameoa mtu kutoka Germany tuseme, hata waishi miaka mia moja hawezi pewa na hiyo si haki nafikiri, na jinsi wananchi walivyo tuambia kwamba kama ni mwanachi wa Kenya awe na haki moja kujihusisha na foreigners. Kwa hivyo mme ama mke wa Kenya anaweza kuolewa ng'ambo na bora tu aishi hapa miaka miwili wanaweza kuomba. Kule kumpa ama kumnyima iwe ni sababu fulani. Kwamba huyu mtu anajulikana si mtu straight, ni mtu ana-deal na drugs na mambo mengine hayo, lakini kusiwe ni kwa sababu yule aliolewa ni wa kike ama kiume.

Pia tumeyazungumzia kuhusu jinsi vyama vya kisiasa wangekuwa regulated. Wasiwe wanaenda kivyao. Tumesema vyama ambazo vitakuwa mwanzo, Tume ya uchaguzi ndiyo itakuwa ni licencing ya registration ya political parties. Tuna propose itoke kwa Registrar of society kwa sababu kikundi ya tuseme vijana wa Youth Groups kama society inakuwa registered under the same as a political party kwa wakati huu. Na tunaonelea hiyo, inapatia political parties more or less freehand kama societies tu. Na wao ndiyo wanajihusisha na uchaguzi na wao ndiyo wataendesha wananchi vizuri ama watawapoteza. Na kwa hiyo regulation ya political parties mpala articles 6 zinazungumzia haya. Jinsi wangekuwa regulated mpaka hata kuwapa pesa wengine wale watakuwa wamepata at least 50% ya national votes, kwa sababu tulikua tumesema chama itakuwa inapigiwa kura pia. Ikipata 5% ya elections watakuwa eligible kwa kupatiwa pesa na serikali ili chama ambacho kiko usukani ambayo sasa inaongoza ama ambayo itakuwa inaongoza wakati wowote, isiwe inatumia mali ya serikali peke yake, lakini ilazimike kwamba budget iweke pesa fulani ya vyama, nusu ya hiyo pesa itakuwa divided kwa parties equally, 50% ya hiyo pesa ambayo itakuwa imewekwa. Na hiyo 50% ingine itakuwa on the proportion of the votes ambazo umepata. Kwa sababu ukisema yote iwe on the basis of proportion of votes, pengine ni chama kimoja kitachukua karibu yote.

Uchaguzi wa vyama katika uongozi wa chama fulani lazima kuwe kuna taratibu fulani paia. Kusiwe ni freehand. Internal elections yapasa pia iwe regulated.

Pia tuna maofisi ya Ombaudsman ambayo ni ya kutetea. Tunauita Public protector ambayo itapokea malalamishi kuhusu abuse of power, kutendewa vibaya, unfair treatment na wafanyi kazi wa serikali na kutofanya recommendations kwa Public Administration na kupromote ile leadership code ambayo tume-propose.

Kutakuwa na Human Rights and Administrative Justice Commission, Gender Commission na hayo yote yatakuwa chini ya Police Complaints Commission ambayo wale watakuwa wametendewa vibaya ya polisi waweze ku-complain kwa hiyo Commission. Na hao wote wataketi katika umbrella ya Human Rights and Justice Commission ili mtu akienda mahali fulani anamalizia mambo yake yote huko. Wasiwe ni watu ambao wanakaa kwa different desks, ili mtu asiwe akisafiri mahali pengine. Na at least wawe kwa District level kama siyo chini zaidi

Kuhusu mali ya Umma, yaani public finances: rasilmali ya serikali imewekwa detail sana mpaka article 10. Kutakuwa na ile nimesema Economics and Social Council. Pia kutakuwa na Auditor and Controller General, tume-propose iwe imetofautishwa. Controller of Budget. Ili Budget itengenezwe mapema sana, wananchi wahusishwe. Ikuje kuzungumziwa jinsi tunavyo zungumza, kabla ya Budget kuwa presented kwa Bunge, na kuwe kumefanywa amendments following those consultations. Consultation ya Constituency, ya District, ya Group Professional systems and all that ifanywe. Na then kuna Auditor General peke yake. Controller of Budget ni Auditor General. Ziwe ni ofisi tofauti na hizi ofisi ziwe of course na security of tenure na constitutional offices.

Uwezo wa Rais katika hii proposal ambayo tuliweka, kuna articles mpaka 7 ambayo yanazungumzia kuhusu uwezo wa Rais na hiyo uwezo wake wote ni muhimu sana. Yeye ni Commander in Chief of the Armed Forces, yeye ata sign Bills zote ambazo zitapitishwa na Bunge, atakuwa ana-appoint Prime Minister na atakuwa ana-appoint wafanyi kazi wa serikali wa Commissions karibu zote, only that zitakuwa vetted na Parliament na atakuwa anafuata procedure fulani ambayo ina-lay, qualifications na requirements. Na mambo mengine mengi ambayo anatakiwa kuhusishwa kama kiongozi wa taifa, tulifikiria kukiwa na mgogoro kati ya Prime minister na Rais kungetatuliwa vipi? Kutatua migogoro yote ya hao watu wawili Rais na Prime Minister. Na tume weka procedures ndefu sana ya kufanya hayo and conflict resolution mechanism between the President na Prime Minister, in the event that there are such conflicts. Hayo pia tuliyazungumzia kwa hiyo Draft Bill.

Uhusiano wa Cabinet na Bunge. Bunge na Cabinet watajihusisha vipi? Kwa sababu katika hiyo bill tume-recommend kwamba Cabinet itoke kutoka kwenye kwa Bunge lakini waweze kuketi kwa Bunge kama ex-official members ambao hawana votes, na kutakuwa aje kuhusu hiyo relationship ya haya maofisi mbili tofauti. Tuko na articles 10 ambayo yanazungumzia hayo pia.

Kuhusu mahakama na jinsi mahakama ingewezesha kupatiwa nguvu zaidi, na jinsi mahakama ingehudumia wananchi kwa njia ya usawa na ya haki. Articles nyingi zinazungumzia hayo chapter nzima kuhusu hiyo Judiciary. Na katika hiyo ndiyo tuli-recommend mahakama mpya, Supreme Courts badala ya Court of Appeal. Na chairman wa hiyo Court atakuwa ni Chief Justice. Lakini pia tume-recommend kwamba katika hiyo mahakama, kusiwe na Judge yeyote ambaye yuko kazini wakati huu. Kuwe na Ma-judges wapya wote, kwa hiyo Supreme Court, kwa sababu ni Court mpya. Ianzishwe na watu wapya ambao hawakuchafuliwa kwa maisha ya kiserikali, lakini wale ambao wako wataingia Court of Appeal.

Kwa hivyo kwa sababu tume-recommend Chief Justice awe ni kiongozi wa hiyo mahakama na tumesema ianzishwe upya ina

maanisha kutakuwa pengine na Chief Justice mwingine wakati Katiba itakuwa imekuwa adopted ili wananchi na watu wa Kenya waweze kujianzisha na watu wapya ambao watakuwa na new leadership code.

Jinsi nilivyo waambia, hiyo leadership code ni detailed sana na ni annex kwa hiyo bill. Ni one of the annexes. Procedure yake ni detailed kabisa na tuseme kama mahakama, pale ndiyo mahali maisha ya binadamu wote inatakiwa iangaliwe zaidi. Ukidhulumiwa ni pale ungeenda, mali yako ikiibiwa ni pale ungeenda, na kama hiyo haina njia ya usawa na haki, hakuna mahali pengine ambapo usawa utapatikana. Na nidyo sababu tume-forcus kwa Judiciary sana kwa sababu ya umuhimu wake, na umuhimu kwa njia ya kitaifa.

Kama kuna Ma-Judges hatuna complaints against them at all, kwa complaint authority yeyote, Attorney General, ama Law Society, ama Complaint Committee. Wao watahitaji ku-sign tu hiyo leadership code mpya na waendelee na kazi yao. Na cha kwanza katika hiyo leadership code ambayo kitakuwa kina kuwa signed na leaders, viongozi wote, baada ya hii Katiba kuwekwa mahali na kuwa adopted, ni pamoja na MPs, Minister, Constitution office holders and Civil Servants from the rank of P.S. Ya kwanza ni uwajulishe wa-declare mali yao yote na kila mwaka waweze kupeana mali yao. Kwamba hii mwaka ulipata mali fulani, kama kuna mali uliongeza ili kusiwe unaamuka leo, kesho unamuona huyu mtu ana mali nyingi, amepata wapi? Hujui. Kama hutaki kujulisha mali yako basi unaacha kutafuta uongozi, ujitetee kwa njia kwa ki-corruption yako na sheria ikikupata ni bahati mbaya. Lakini kama unataka kuingia kutafuta uongozi, hadi upite hiyo sharti ya ku-declare your wealth.

Pia Draft inazungumza kuhusu ardhi na environment in general na tume-propose, National Environment Management Commission. Saa hizi tuna NEMA, National Environment and Management Authority, lakini ni jina tu. Most of the functions are there lakini tumefanya hiyo Commission iwe Constitutional Commission ambayo hakuna yule anayeweza kuja kesho na kuiondoa. Iwe ni Constitutional Commission naiwe led by a Director General.

Pia kuhusu ardhi tuli-recommend wananchi kuwa mtu yeyote wa kigeni asiwe anamiliki ardhi. Hiyo tulisikia kwa kila mahali pia. Awe anaweza ku-lease tu, apatiwe leasehold title ya miaka isiyo zidi tisaini na tisa. Wakai huu naona lease holds ambazo ziko mpaka 999 years, karibu karne kumi. Lakini mwananchi ndiye atakuwa mwenye ardhi na ardhi yote ambayo lease yake imekwisha inarudi kwa National Land Commission na kama ni ya mgeni, ni lease tu atapewa tena na siyo freehold title.

Pia tumeyazungumzia kuhusu jinsi Katiba ingeheshimiwa na wananchi kuifwata inavyo takikana, na jinsi wananchi wangeweza ku-protect Katiba. Pia tuliyazungumzia kwa hii Draft Bill.

Kwa ufupi hayo ndiyo yale ambayo yamo katika Draft Bill. Kutakuwa na copy ya Kiswahili. Hii short version tuna Kiswahili na Kingereza. Na ile long version itakuwa na Kiswahili na Kingereza pia sasa iko kwa publisher. Nafikiri pia ile imechapishwa kwa gazeti iko kwa Kiswahili na Kingereza. Pengine hamjaona ya Kiswahili bado, ya Kingereza ndiyo mliona. Ya Kiswahili pia walipewa kwa media, hawaja-release, wata-release any time now. So mtayaangalia hayo pia. Na kama kutakuwa na

suggestions ambayo mna-feel strongly kwamba ingeongezwa kwa ile iko ama ingepunguzwa, ama tunge modify that which we feel strongly about. Unaweza kuiandika na mpatie coordinator. Itafika ofisi yetu before the 20th. At least mko na advantage tumeanzia na kwenu. Nafikiikiri pale nitamalizia mimi itakuwa ni tarehe 18 na watukuwa na siku mbili, tatu. Kwani ni lazima 20th iwe deadline ya kila mtu. At least nyinyi mtakuwa na siku kumi hivi ama karibu wiki mbili. Mhakikishe muangalie na m-comment kama mnaona hayo yangefaa kufanywa vingine. Asanteni. (clapping)

Let me take this opportunity to recognize the presence of District Officer 1 wa wilaya hii ambaye anawakilisha Bw. D.C. Madam karibu. Kwa hivyo kama kuna quick reactions ambayo mgependa tuyazungumzie jinsi tulivyozungumzia mengine, nafikiri wakati huu ningewaalika, muulize.

**Peter Mulavu**: Asante. Nafikiri Bw. Commissioner nilikuwa nauliza hivi. Kama vile umesema ukijibu swali la mwenzetu pale-- Mimi ni Peter Mulavu mmoja wa waalimu wa civic. Nilikuwa nauliza hivi, vile tunatarajia kuwa na hiyo National Conference, je ungetuelezea nini kuhusu kama wengine katika wale ambao tutatUmma huko ama pengine Wabunge, ama pengine Commissioners, hawatakuwa waaminifu walete fujo ama wakose kuelewana. Wakati wa National Referendum utakuwa nini? Ame pengine wakikosa kuelewana katika Conference? Kwa sababu umetueleza the positive side of the process, what of the negative?

**Jacob Kitheka**: Nilikuwa nimezungumza tena. Jina langu ni Jacob Kitheka na nimesema vile vile nilikuwa mwalimu wakati wa review, nikiwa Chairman mmoja katika CPOs wa hapa. Yale tumeelezewa yote ni mazuri sana na mimi nilikuwa nikitazamia kwamba shabaha yake ni ikiwezekana kila mwananchi ajue haya. Na mwananchi kujua haya moja ni kumpelekea na kumsaidia kuelewa. Lingine ni kumpa copy. Kile ningeuliza ni kwamba kama copies zonaweza kupatikana na kama zitauzwa, kama zinaweza kuuzwa kwa bei ambayo itazifanya zifike kule zinatakikana kufika.?

**Joseph Mutonga**: Thank you very much ,I am Magithi Mutonga. I have one pressing issue I would like you to clarify to us and this is the animal that the Constitution is giving us to reclaim the Provincial Administration. I am personally very worried that you are abolishing the Provincial Administration and leaving a very big vacuum in the sense of two things. One, security and two, the extra Judicial service that is given by the Provincial Administration.

Let me elaborate on the security part of it. We know that the Provincial Administrator especially PC, the Chief and the Sub-Chief, they form a very big function of security right in the village. If the village canteen is broken into, the Sub-Chief mobilizes his askaris and one way or another they solve those problems in the village. This is a function that in a more practical sense it cannot be done by the regular police men. For instance if I were to give you an example ------(end of tape)

--in 60 KMs we have one Police Station here and the other one is in Kiso. The regular Police men cannot provide security in the area between that 60 KMs and sometimes even larger areas, but this is a function that is done by the Provincial

Administration. So when we remove them and the Constitution does not give us a replacement for these, did the Commission take into consideration what is going to replace these functions? Otherwise I am seeing a very big blunder that wananchi may be committing. I know Kenyans are fed up with the Provincial Administration and maybe because of emotionalism, they did not think of what to replace this function that is done the Provincial Administration.

Secondly, I am also worried about the extra-judicial service that is given by the Provincial Administration. Back in the village, if you cut Wanjiku's tree, Wanjiku does take you to a Court of law because you cut her tree. This is taken to the area Chief who sometimes is forced even to give a fine and the case is out of that area. The system that we have of elected people who are coming to replace the present system, clearly cannot do this. When a man beats his wife sometimes, these are things that are sorted out at the village level by the Sub-Chief and sometimes by the Chief and yet the system that we bringing to you to replace, cannot do this exactly because the Constitution does not give them the power to do this. So did the Commission in addition to taking the views of the wananchi, did they take this into consideration. Thank you.

**Com. Nunow**: Asanteni sana. Nafikiri hayo yote ni muhimu na ni kwa sababu ya hiyo ndiyo kwamba hii Draft baada ya hapo itaenda kwa National Constitutional Conference.

Kwa hivyo ningeanza na swali la pili kuhusu Provincial Administration. Mwanzo tulijaribu iwezekanavyo kuhakikisha kwamba maoni ya watu ndiyo tu-relect. Ni kweli kwamba kwa miaka karibu arubaine wananchi wamejua Provincial Administration na inafanya kazi muhimu sana lakini juu ya hiyo kazi pia and common interaction yao kila siku, ndiyo ilifanya watoe hayo maoni. Kwa sababu wanaona Chief kila siku akonao, wakiteleza kidogo anawashika, wakitengeneza changaa ako nao. Lakini mwanzo ilikuwa sichukui maoni yao ya kwanza, iwe kwa Report. Ya pili ikawa, maoni yao utaweka aje kwa Katiba ndiyo tumefikiria jinsi ya Devolved Government. Chapter nzima inzungumzia Devolution of Power, kutoka Village Councils hadi Provincial Councils, ambayo kutakuwa na Location Administrator. Kutakuwa ambao ni Division level, nikama ile tu ambayo ilikuweko.

The fact that our recommendation haikuenda mbali na ile iko, inamaanisha kwamba tunatambua umuhimu yake. Locational Administrator the Divisional level, District Administrator, Provincial Administrator na at the middle ground, tume re-commend hayo yawe elective positions except the Provincial Administrator ambae atakuwa elected internally by other District Councils. All the District Councils of the Province coming together forming an electoral collegue ambaye watampigia kura mmoja ya wao. Ama momja ya wao kutoka kwa hizo Councils. Ambaye pia atakuwa amechaguliwa kuja kwa hiyo Council mara ya kwanza. So si mtu ambaye ametoka nje. Lakini hiyo haimaanishi ya kwamba haina weaknesses ama haitaweza kufikiriwa zaidi na kuipatia nguvu ama kuibadilisha.

Nilisema kwenye Draft, recommendations maybe amended, maybe completely abandoned or maybe completely retained and ammended. Those are three options ambazo this Bill has to be subjected to. Na nafikiri we will not have justice kama hatukujaribu ku-reflect jinsi tulivyo ambiwa. Jinsi tulivyo ambiwa kama inafaa ama haifai itakuwa ni swali la siri la kufuata hiyo.

Kwa hivyo wale ambao wana maoni ambayo wanadhania jinsi hii Devolved Governemt, hii Council, inaweza kuwa replacement ya Provincial Administration, ama haitaweza kuwa replacement because of ABCD, nafikiri ningeomba muandike, in your feedback, please write it. If we knew we didn't need any more input at all hatungekuja. Tungengoja Conference na tupeane. The fact that tumekuja na tunawaambia mna deadline ya tarehe 20, ina maanisha kabla ya conference tarehe 28, we can revise this Draft in the light of watu wamesema aje. Kwa sababu tunaenda katika kila Constituency tena in the next two weeks, from now until the 17th.

So please write and for it to get there very fast, give to the Coordinator. Because you need a fax or travel to Nairobi and take it or use your own machinery to ensure that it gets there. Kwa sababu ukiiweka kwa posta inaweza lala.

Kuhusu conflict resolution ya Conference. Ni kweli imeonyeshana mezungumzia positive side because the Draft Bill is positive. We don't anticipate complications, lakini kuna mechanism ya ku-resolve stalemates. Mwanzo ilikuwa kwamba for an issue to go to the Constitution it needed 2/3 of all members. 2/3 of all members is quite a high number. And some people can subotage the exercise by refusing to go there. Members of the Conference ambao hawataki jambo fulani liende, wanaweza kukataa kwenda kule. Saa zile members ambao watakuweko hawatakuwa wamefika two thirds. Ndiyo Parliament imefanya amendment ya hiyo sometimes this year, nikasema 2/3 of those present and voting.

So watu wale ambao hawataki kwenda hawataweza ku-sabotage the exercise. Wale ambao wako ndiyo watatoa maoni yao na ndiyo watakae piga kura. Kwa hivyo kama jambo halitapata consensus, litakuwa subjected kwa voting. Na kama jambo ni ya Constitutional issue na haikupitishwa by those two thirds. Na two thirds of those present voters agree that this should be agreed by Kenyans, two thirds of those who are there, waseme hii iamuliwe na wananchi wote, that will be an item for referendum. Hiyo ndiyo itarudi kwa wananchi kwa kura ya maoni. Na ile itakuwa imekubaliwa itaendelea, ile itakuwa imekataliwa itatolewa. So although the focus is consensus, kama jambo halitapata consensus tuna mpango wa kuacha hiyo jambo kwa siku moja ama at least 24 hours, 48 hours watu waifikirie, wa-reflect, kisha tu-introduce tena. Kwa sababu kama wakati mwingine unachemka sana, hautakuwa very rational. Lakini ukisha poa na umepumzika, unaweza kuona point ambayo haukuwa unaiona.

Kuhusu copies ya Draft Bill, kwa wakati huu, mtaendelea na mtaitumia ile iko kwa gazeti, hiyo pull-out. Lakini Draft Bill haitauzwa, itakuwa available, Draft Bill plus the report free of charge pengine pia haitatosha watu wote. Pengine mpaka copies 200, 300 kwa kila Constituency kwa sababu ya masilahi, kitabu hiki mwingine anaweza kukisoma na watu wengi. Na hiyo tulionelea kwa ile issues and questions booklets. Tuliona (inaudible) kwa wananchi jinsi ilivyo tembea.

Asubuhi mwanzo kuna mtu aliuliza kuhusu kujulisha watu Katiba, tume-suggest kwa hiyo Reports kwamba Katiba ifundishwe kwa shule both Primary na Secondary na mpaka Vyuo vikuu na pia kwa njia ya pesa, iwe inauzwa pesa kidogo sana ikisha kuwa published. Na ya mwisho iwe kwa lugha ambayo inaeleweka na kila mtu. Hiyo ndiyo approach ambayo tulisema,

ikichukuliwa baada ya miaka kadhaa, watu wengi watakuwa wanajua Katiba. At least the major features za Katiba, siyo details. Details utajihusihwa wakai una mambo fulani unayoangalia. Lakina tunaonelea kila mtu aweze kuwa na copy yake kama reference book. Ili baada ya miaka kumi, kumi na tano karibu wananchi wote wawezee kujitetea wakitumia Katiba yao. Na isiwe kwamba ni lugha ambayo mawakili tu wanaweza tafsiri.

Nafikiri hayo ndiyo yalikuwa yale maswali yameulizwa.

**Musili Musyoka**: (inaudible) --- so kitu cha kwanza tunakushukuru for your very able presentation this morning and this afternoon because although we had a very small crowd, this is the crowd that actually disseminated the information all over the District. Because the majority of this people are 3C's members and CEPS, they understand the languange that we are talking about, they are aware of the duty that is bestowed upon them from now on, though we are going to talk about that later.

So I think that before I proceed I would like to invite our D.O.1 to say maybe a few words, although she came a little late, we had a long session, we had presented our Constitutional Report and she found us on the presentation of the Draft Bill and now we are winding up Kwa hivyo labda madam, she is very much aware of what we are talking about. Kwa hivyo ningemuuliza madam azungumze na sisi kidogo kwa sababu hawa ni wananchi wake na hata sisi pia na yeye labda atuonyeshe muelekeo kabla hatujafunga huu mkutano wa leo. Madam tafadhali.

**Madam Rose Wakibia- D.O.1**: Asante sana Coordinator wetu Bw. Musyoka, Com. Dr. Nunow, other officials na wananchi hamjambo?

**Audience**: Hatujambo.

**Madam Rose Wakibia- D.O.1**: Kwamba kabisa nina omba radhi kwa sababu ya kuchelewa kwa sababu ya kazi nyingi ofisini. D.C pia hayuko, imenibidi niwe pia kwa ofisi kidogo. Na bila shaka hicho kikao chenu cha kwanza, wakati watu walikuja kutoa maoni tulikuwa pamoja na nafikiri leo pia ni siku ya muhimu sana kusikia waki-respond kwa ile Draft kwa kuwa ni yale maoni mmeweza kutoa kwa grassroots hata kuhusu sisi kuwa hatuko kazini pia, ni maoni mazuri pia kwa sababu tutakuwa mahali pengine. Kwa hivyo nafikiri kazi ya Katiba vile Commissioners mnafanya ni ya maana sana kwa sababu mnachukua muda, hamulazimishi watu kwa nguvu, eti Draft ndiyo sasa hii na inatufaa, hapana. Mnarudi kwetu tena ndiyo muwe na hakikisho kamili ya kwamba kila kitu ambacho mwishowe Katiba ile itatuongoza siku za mwishowe ni Katiba ambayo itakubalika na kila mwananchi na kila mtu kwa sababu Katiba inahusu maisha yetu ya uchumi ya siasa na ya jamii. So it will be a very holistic Constitution, kwa hivyo nafikiri mwendelee namna hiyo hiyo, tuko pamoja na ninajua vile mnahusisha wananchi mwishowe mtakuwa na Katiba ambayo itaweza kutusaidia na kutupatia muongozo mwema. Kwa hivyo kwa hayo machache nitawatakia mema hata kesho mnaelekea South, tuko pamoja na nyinyi. Asanteni sana. (clapping)

**Musili Musyuoka**: Asante Madam D.O.1 sasa kama hakuna mtu ako na jambo ambalo linamuasha, tutaendelea karibu kufunga mkutano sasa ni saa saba karibu unusu. Kuna jambo kabla sijafunga mkutano? Nafikiri sasa mnafahamu kiini cha Katiba yetu ni nini. Commission haina Katiba. Katiba ni ya watu, people's choice kwa hivyo yale maoni mmerudishiwa, na tunasema kutoka hapa tuirudishie mashinani, turudishie watu watwambie sisi watu wa kuandika, imeandikwa vile mliandika maoni ama vipi. Kama mna mageuzo mseme ndiyo mnasikia Commissioner akisema kama kuna watu wenye maoni tofauti, wanataka kuongeza waongeze, wapitishe kwa Coordinator, ndiyo tupeleke tena, tupeleke kwa Commission ipelekwe kwa National Constitutional Conference. Halafu ile ya mwisho itajadilianwa huko ndiyo itokee ile maoni yote ya Wakenya kwa sababu maoni ni ya Wakenya, Katiba ni ya Wakenya, si ya mtu fulani, si ya watu fulani, ni ya sisi sote. Kwa hivyo nafikiri hapo hakuna mtu atasema oh! hi Katiba ni ya akina fulani. Hiyo fikira limetoka, kwa sababu kama vile Madam D.O amesema tulikusanya maoni hapa tukapeleka, sasa maoni ile ile imerudi hapa na tunataka tuirudishe pia kabisa kwa watu. Kutoka leo tutarudi tena mpaka huko kwa vijiji, tuirudishe tena.

Kwa hivyo nauliza wale 3C's members wako hapa, wale CEPS wako hapa mbaki na wale wengine wakiondoka, mbaki tuongee vile tutakutana ili tugawane ile kazi ambayo imebakia. Ile mmesikia Commissioner akisema ya three weeks. Tujue tutaifanya namna gani, ili ile ma-reporti yote itatoka kwa watu kulingana na hii reporti ambazo zimetokea. Tuikusanye watoe maoni pia, watoe mageuzo yao na tuikusanye tuipeleke tena kwa Commission nayo Commission ipeleke kwa National Constitutional Conference.

Tuko na bahati sasa katika wale delegates tulichagua tuko na wawili hapa, simameni muonekane. Huyo Bwana anaitwa Bw. Robert Maloki ni delegate mmoja, huyo Com. Nunow na huyu madam naye anaitwa Mwikali Mutunga pia ni delegate kutoka hapa. Kuna mmoja amebaki, yeye anaja Nairobi kwa hivyo tuko watatu. Sisi hatuna shida hapa, watu wanangojea tu ile siku nimewaambia na wakati ukifika kama huu, waje wawe nasisi ili wasikie tunaendelea namna gani, ili ile siku ikifika ya kuenda kuwakilisha sisi huko Nairobi, wao wawe tayari wajue wananchi wanasema nini ndiyo waweze kuzungumza. Lugha ya wananchi. Kwa hivyo ndiyo naona wameanza kuja. Yule wa Nairobi ako njiana, labda atakuwa nasisi kesho. Kwa hivyo iko namna hiyo.

Kwa hivyo isipokuwa wale tu nimetaja CEPTS na 3C's wale wengine nawashukuru nyote, wale wamekuja na asante sana. Tutaomba halafu wale Ma-CEPTS na 3C's tutabaki ili tujue muelekeo wetu utakuwa namna gani kutoka pale nasema ni asante, wale wengine tutazidi na kuonana. Asanteni sana. Nafikiri mtu mmoja tu asimame atuombee. Nani ako na roho? Tafadhali Mulavu asante.

**Peter Mulavu**: Wakati huu mwema Mungu Baba uliye juu Mbinguni tumerudi kwako ili kutimiza ahadi yetu kwako. Tulipokuwa tukianza mkutano Mungu, tulikuuliza ukawa pamoja nasi na tukaahidi kwamba tukifikia mwisho tukiwa chini ya uongozi wako na baraka zako tutakushukuru. Kwa yale yote ambayo Baba tumeongea, si kwa ajili yetu sisi wachache ambao

tuko hapa lakini kwa ajili yetu na watu wetu wote wa nchi ya Kenya. Utubariki na Roho wako Mtakatifu akatuongoza pamoja nawale ambao hatuko nao hapa. Viongozi na Commissioners ambao wako hapa tunataka kuwaombea wakienda kwa safari tofauti kwa ajili ya kazi kubwa ambayo umeweka mbele yao. Tunaomba baraka zako zikaandamane na wao.

Utusamehe lolote mbaya ambalo tumefikiria ama tukiwa mahali hapa. Katika jina la Yesu tumeomba.

**Audience:** Amen

The meeting was closed at 1:50 pm.

**&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&**